




**Utouh** alitaja tatizo kubwa linalotishia uhai wa taifa

UKURASA 2


MAISHA
Nipashe Jumapili
Baba, Mama na Mwana
MAISHA NI NYUMBA
JIPAMBE NA SUPU YA MABOGA
Rembesha uzio kupendezesha nyumba yako
KATUNIKA
Tunaruka hivi na jeans 2023

UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Mei 28, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581324

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




# Kigwangalla matatani

• **Kupandishwa** kizimbani, mlinzi wa kiwanda chake naye kushtakiwa...*Ukurasa 3*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### ZITTO KABWE ALIA NA MAKAA YA MAWE

KIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe amesema serikali inatakiwa kuangalia uwezekano wa haraka wa kutengeneza reli ya kutoka...

UKURASA 3

### Chongolo: walioanza fujo CCM watakatwa






Rais Samia Suluhu Hassan akipokea tuzo ya pongezi na shukrani kutoka kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla iliyotolewa na Chama cha Makatibu Mahsusi Tanzania (TAPSEA) pamoja na Menejimenti ya Watunza Kumbukumbu na Nyaraka (TRAMPA), baada ya kufunga mkutano wa kitaaluma wa TAPSEA na TRAMPA, Fumba Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Samia atoa angalizo kuvuja siri za serikali

UK 2


**MICHEZO** USM ALGER HATARI KWA KONA, BEKI... UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Wateja wakinunua samaki wa kukaangwa waliokuwa wakiuzwa katika eneo la wazi bila kufunikwa, huko Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wa afya zao kutokana na kitoweo hicho kuingia vumbi na nzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Utouh alitaja tatizo kubwa linalotishia uhai wa taifa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, ameona ombwe linalotishia uhai wa taifa kwa sasa la kupungua kwa uadilifu, uzalendo na kukosekana kwa uwajibikaji wa watanzania, akishauri wanazuoni kubuni na kutafakari njia sahihi za kulishughulikia.

Utouh ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, alikuwa anazungumza jana na wasomi mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), alikokwenda kuzindua kamati ya ushauri wa uhusiano na sekta binafsi/soko la ajira, iliyopewa jukumu la kushauri na kutoa mchango wake katika mradi wa kitaifa wa elimu ya juu wa mageuzi ya kiuchumi (HEET).

"Kamati ya ushauri na uhusiano wa sekta binafsi, soko la ajira ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, mna kazi muhimu sana ya kukishauri chuo na kukiunganisha na wadau wengine wa ndani na nje ya nchi ili kuboresha utoaji wa elimu kwa maendeleo endelevu katika nyanja zote za nchi yetu.

"Niombe kamati hii ichukue jukumu moja muhimu, ambalo ni kiunganishi na majukumu mengine ya msingi mliyonayo. Na jambo hilo si lingine bali mjitahidi sana kubuni na kutafakari njia sahihi za vyuo vyetu vikuu, ikiwamo Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, kutafuta jinsi ya kushughulikia tatizo linalotishia uhai wa taifa la uhuishaji wa uadilifu, uzalendo na ukosekanaji wa uwajibikaji wa watanzania.

"Tunaweza tukafundisha, watu wakawa na huo ujuzi lakini kusema kweli bila kuwapo uadilifu, kukawapo na uzalendo na watu wakaelewa kuhusu uwajibikaji, bado wahitimu wetu watakabi kujifunza. Uadilifu, uzalendo na uwajibikaji ni muhimu na una maana pana kwa taifa, kwa sababu ni muhimu sana kwa soko la ajira," alisema.

Kamati hiyo ya wanazuoni inaundwa na Mkuu wa Tume ya TEHAMA nchini, Dk. Mkundwe Mwasaga, Msajili wa zamani wa Hazina, Dk. Oswald Mashindano, Agapiti Manday, Anthony Chamanga, Prof. Fedy Kilima, CPA (T) Josephat Kisamalala, Laurine Kilemwa, Godfrey Ng'urah na Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Akiba na Mikopo (SCCULT), Hassan Mnyone.

Utouh alisema Mradi wa Kitaifa wa Elimu ya Juu wa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), unawezesha kufanyika mabadiliko makubwa ya mitaala sambamba na uboreshwaji wa miundombinu ikiwamo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alisema kwa maono yake, anaamini nafasi ya ubora wa elimu ya juu itaamuliwa kwa kiwango cha matumizi ya TEHAMA, ikiwamo kubuni mitaala inayoakisi maendeleo. "Kwa ujumla vyuo vyetu vingi, vimeendelea kutumia njia za asili na za kizamani katika kutoa mafunzo yake, yaani mwalimu na mwanafunzi lazima mwonane katika chumba kimoja cha darasa. Ninatambua vyuo vya elimu ya juu nchini vinavyotoa elimu yake kwa kutumia TEHAMA, bila ya mwalimu na mwanafunzi kuwa pamoja katika chumba cha darasa. Tungepanua huo wigo juu ya TEHAMA," alisisitiza Utouh.

Mradi huo wa HEET unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania, chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB). Dhima kuu ya mradi huo ni kuwa na elimu inayoendana na soko la ajira.

Awali, akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa HEET chuoni hapo, Mratibu wa Mradi huo, Prof. Fredy Kilima, ambaye ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala, alisema mradi huo unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021/2026) na unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania kupitia mkopo wa Benki ya Dunia , ambapo chuo hicho kimepatiwa Sh. bilioni moja.

Alisema kuwa kupitia mradi huo, chuo kimelenga kuboresha mambo mbalimbali ikiwamo kuboresha mazingira ya kujifunza na ufundishaji, kwa kujenga majengo mapya, kufanya marejeo ya mitaala mipya yenye kuleta tija katika soko la ajira, kuwajengea uwezo wanazuoni kuwa wabunifu na kumudu kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano na kuhamasisha matumizi ya teknolojia.

Baada ya uzinduzi huo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (Taaluma, Utafiti na Ushauri), Prof. John Safari, alimhakikishia Utouh kwamba mradi huo utatekelezwa kwa ufanisi mkubwa, wenye kuleta mabadiliko yanayohitajika hasa katika kuongeza matumizi ya TEHAMA, taaluma, utafiti na ushauri.

Kwa mujibu wa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Prof. Alfred Sife, tayari wameanza rasmi mchakato wa kukusanya maoni ya waajiri katika bodi zinazosimamia taaluma na utaalamu, sekta ya umma na binafsi, wahitimu na wanafunzi, kabla ya kuifumua mitaala 15 na kukuandaa programu mpya 11, zitakazoamua hatma ya wanaohitimu elimu ya juu kukabiliana na soko la ajira.

Prof. Sife alieleza kuwa hatua hiyo ya kurejea mitaala iliyopo na kuandaa mipya ni muhimu katika kipindi ambacho soko la ajira limebadilika, kwa maana ya kuwa na mahitaji mapya ya ujuzi na maarifa.

# Samia atoa angalizo kuvuja siri za serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan amewataka makatibu mahsusi na watunza kumbukumbu na nyaraka kuzingatia weledi wa kazi zao na kutotoa siri za ofisi.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akifunga mkutano wa kitaaluma kwa makatibu mahsusi Tanzania na menejimenti ya watunza kumbukumbu na nyaraka.

Katika mkutano huo, Rais Samia aliwataka watendaji hao kuzingatia miongozo na mipaka ya kiutendaji, akisema kwa yeyote atakayekwenda kinyume cha kiapo cha uadilifu wa kazi, hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yao.

Alisema nidhamu, uadilifu na utunzaji wa siri unaongeza tija na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao ya kazi kwa maendeleo ya nchi.

Dk. Samia pia aliwaahidi watendaji hao kuwanyanyua na kuwaendeleza kitaaluma ili zinapotoka nafasi za uteuzi, wazipate.

Alisema utaratibu huo wa kuwafanyia mafunzo maalum watendaji hao nje ya maeneo yao ya kazi ni mzuri na unapaswa kuwa endelevu.

"Fursa pekee kwa kada hizi ni hii kutoka nje ya ofisi zenu maana hamna fursa za kutoka kama kada zingine,"alisema Rais Samia.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, aliwataka watendaji hao kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria na kiapo walichoapa cha uadilifu wa kazi.

"Lazima kuhakikisha watendaji kuzithamini kazi za makatibu muhtasi na watunza kumbukumbu kutokana na umuhimu wao mkubwa hasa wa kuwalinda viongozi," alisema.

Makamu wa Rais alisema kufanyika kwa mkutano huo Zanzibar ni faraja kubwa. Pia imeonesha hadhi ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa sababu wapo baadhi ya watanzania ni mara yao ya kwanza kufika visiwani hapa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema katika kuboresha viwango vya katibu mahsusi, Chuo cha Utumishi wa Umma kimeboresha mitaala yake.

Alisema katika kushughulikia matatizo ya kiutumishi za kada za makatibu mahsusi na watunza kumbukumbu na nyaraka, ofisi yake imeboresha miundo yake ambayo itaanza kutumika Julai mwaka huu.

Alisema serikali imetoa vibali 512 za ajira mpya kwa makatibu mahsusi na 443 kwa kada ya watunza kumbukumbu na nyaraka.

Mwenyekiti wa Chama cha Makatibu Mahsusi (TRAMPA), Devota Mrope na Mwenyekiti wa Chama cha Watunza Kumbukumbu na Nyaraka (TAPSEA), Zuhura Songambele, kwa nyakati tofauti walisema hakuna maendeleo bila kuhakukuwa na kumbukumbu hasa ikizingatiwa historia ya maaisha imejaa kumbukumbu.

Mlope alisema: "Tunakuahadi kwamba hatutatoa siri, hatutoiba wala kuuza nyaraka na yoyote atakakwenda kinyume cha kiapo alichoapa, atabeba msalaba wake mwenyewe."

Alisema watazingatia weledi na miiko ya kitaaluma na kuahidi kutekeleza maagizo ya kutunza siri na nyaraka za serikali na kuhakikisha wanamsadia Rais Samia katika utekelezaji wa majukumu yake kutoa huduma bora kwa wananchi.

Wakielezea matatizo yanazoikabili kada hizo, alitaja kuwa ni utekelezaji wa muundo wa utumishi kwa waajiri na maofisa utumishi na idadi ndogo ya wanataaluma waliofika katika mafunzo hayo kutokana na baaadhi ya waajiri kutotoa rukhsa.

Alisema sababu ya kuvuja siri ni kusimamiwa na baadhi ya watu ambao hawajasomea utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka licha ya kuwapo vyuo mbalimbali vinavyotoa elimu hiyo.

HABARI KITAIFA

# Kigwangalla kuburuzwa kortini tuhuma kumjeruhi mlinzi wake

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linatarajia kumfikisha mahakamani Mbunge wa Nzega Vijijini (CCM), Dk. Hamis Kigwangalla kwa tuhuma za kumpiga na kumjeruhi mlinzi wake, Jumanne Omary (66).

Dk. Kigwangalla ambaye ni mmiliki wa kiwanda cha kuchakata pamba kiitwacho Mwalujo Ginery kilichopo Kijiji cha Mwalujo wilayani Kwimba mkoani Mwanza, anatuhumiwa kutenda kosa hilo Mei 22 mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, inaeleza kuwa hata mlinzi huyo atafikishwa mahakamani kwa tuhuma za kutoa taarifa za uongo.

Kamanda Mutafungwa alisema Dk. Kigwangalla anatuhumiwa kumpiga na kumjeruhi mguu wa kulia mlinzi wake huyo ambaye pia anashikiliwa na jeshi hilo kwa kutoa taarifa zinazodaiwa za uongo kwamba alijeruhiwa kwa kupigwa risasi na mbunge huyo.

Kamanda Mutafungwa alieleza kuwa katika kiwanda hicho kulitokea wizi wa mali mbalimbali za Sh. milioni 28.5, hali iliyozua mgogoro baina ya mmiliki wa kiwanda hicho na mlinzi wake.

Alidai kuwa Mei 22 mwaka huu saa 11 jioni, Dk. Kigwangalla alifika kiwandani kwake ambako kulitokea majibizano kati yake na mlinzi.

Alisema siku hiyo hiyo mlinzi huyo alitoa taarifa kituo cha polisi kuwa alishambuliwa na kupigwa risasi katika mguu wake wa kulia na kupatiwa PF3 na kwenda Hospitali ya Wilaya kwa ajili ya uchunguzi.

Kamanda huyo alisema kuwa Dk. Kigwangalla alihojiwa na polisi na kufunguliwa mashtaka ya kushambulia na sasa yuko nje kwa dhamana na anatarajiwa kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka yake.

Vilevile, taarifa hiyo ya Jeshi la Polisi ilieleza kuwa baada ya uchunguzi kufanyika, iligundulika kuwa mlinzi huyo hakuvunjwa mguu wala kujeruhiwa kwa silaha ya moto.

“Hivyo, mlinzi huyo naye anashikiliwa na kufunguliwa jalada la uchunguzi kwa kosa la kutoa taarifa za uongo kwa ofisa wa polisi na kuzua taharuki kwa jamii kuwa amepigwa risasi. Hivyo, naye anatarajiwa kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka yake,” alisema.

Kamanda Mutafungwa alieleza kuwa upelelezi wa kesi hizo mbili unaendelea na utakapokamilika watuhumiwa wote wawili watafikishwa mahakamani huku uchunguzi wa tukio la wizi katika kiwanda hicho ambao uliripotiwa katika Kituo cha Polisi Kwimba unaendelea kufanyika na taarifa zaidi itatolewa pindi utakapokamilika.

Alisema Jeshi la Polisi linawataka wananchi mkoani humo kuchukua hatua sahihi za kisheria na kuacha tabia za kujichukulia sheria mkononi pindi wanapokuwa na migogoro ikiwa ni pamoja na kushirikisha vyombo vya dola au taasisi zenye mamlaka.



Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi (kulia), akizungumza wakati wa mkutano maalum wa Baraza la Vyama vya Siasa, jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Mwenyekiti wa Baraza hilo, Juma Khatibu na Makamu Mwenyekiti wa Baraza, Anamringi Macha. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# CCM: Walioanza kujinadi kabla ya muda watakatwa

**Na Nebart Msokwa,** MUFINDI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetoa onyo kwa wanachama wake ambao wameanza kujipitisha kwa wananchi kabla mchakato wa uchaguzi kuanza wakiwashawishi wawachague.

Kimesema kitachukua hatua kali dhidi yao ikiwamo kuwaengua katika mchakato wa uchaguzi pale muda wake utakapowadia.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo alitoa angalizo hilo jana alipozungumza na wanachama wa chama hicho wa Mji wa Mafinga wilayani Mufindi mkoani Iringa katika ziara yake ya siku sita.

Alisema nafasi ambazo wanachama hao wamekuwa wakiwashawishi wananchi kuwachagua ni ubunge, udiwani na uwenyekiti wa serikali za mitaa. Alisema muda wa mchakato wa uchaguzi kwa nafasi hizo haujafika.

Hivyo, aliwataka wanachama wenye nia ya kugombea nafasi hizo, kuwaacha viongozi waliopo madarakani wamalize muda wao.

“Ukijipitisha mapema unaturahisishia kazi. Sisi ndiyo tunapitisha na kukata majina ya wagombea. Sasa tukipokea malalamiko tutatunza taarifa zao ili siku ikifika iwe rahisi kushughulika nao. Wewe kama unataka nafasi hiyo endelea kuvuta subira mpaka tutakapotangaza,” alisema.

Chongolo alisema muda wa uchaguzi ukifika kuna utaratibu wa walioko madarakani kuachia ngazi ili kuruhusu mchakato kuanza upya na hivyo akawataka wanachama wa chama hicho kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa.

Katibu Mkuu pia aliwaagiza viongozi wa CCM Wilaya ya Mufindi kuunda mfuko wa mabalozi wa chama hicho utakaowawezesha kuwa na miradi ya kuwaongezea kipato ili watekeleze shughuli zao za kukijenga chama vizuri.

Pia aliahidi kutoa pikipiki 16 kwa mabalozi hao ambazo watazitumia kwa ajili ya kujipatia kipato na kuwasaidia kuwafikia wanachama katika maeneo yao.

“Chama chetu hakina uwezo wa kuwalipa posho mabalozi wote nchini, lakini tunachoweza kukifanya ni kuwawezesha kuanzisha miradi ya kujiingizia kipato,” alisema Chongolo.

Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa CCM, Sophia Mjema aliwataka wazazi na walezi katika Wilaya ya Mufindi kuimarisha lishe kwa watoto wao ili kukabiliana na tatizo la udumavu ambalo linaikabili wilaya hiyo na maeneo mengine.

Alisema baadhi ya wazazi wa wilaya hiyo wamekuwa wakiwanywesha watoto wao pombe za kienyeji aina ya ulanzi, jambo ambalo alisema halifai kiafya.

“Watoto wapate lishe bora ili tuondokane na tatizo hili la udumavu na tupate viongozi na wataalamu bora baadaye ambao watatusaidia kutekeleza miradi ya maendeleo baadaye,” alisema Mjema.

Katibu wa Oganaizesheni wa CCM, Issa Haji Ussi, maarufu Gavu, aliwataka wanachama wa chama hicho kuendelea kulipia kadi zao za uanachama ili waendelee kunufaika na fursa mbalimbali zinazopatikana ndani ya chama.

Alisema kwa sasa chama hicho kinaendelea na utaratibu wa kutoa kadi za kielektroniki kwa wanachama wake ambazo zitakuwa zinawasaidia wenye nazo kupata bima ya afya, zitatumika kulipia mifuko ya hifadhi za jamii na kutumika kama kadi za kutolea fedha benki.

Katibu Mkuu wa CCM na viongozi wengine wa chama hicho ngazi ya kitaifa wanaendelea na ziara katika Mkoa wa Iringa ambako watatembelea wilaya zote kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo, uhai wa chama na kusikiliza kero za wananchi.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KILOLO**

**Kituo cha KILOLO Mkoa wa IRINGA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na. 05/2023**

**Jina la mdai ANTONY EXPEDITO LWIMBO**

**Jina la mdaiwa HARUNA MUHANGA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za utaratibu Madai Katika Mahakama ya Mwanzo)**

**Kwa: HARUNA MUHANGA**

Kwa kuwa mdai/wadai ametoa/wametoa madai yake/yao kwamba **UNAAMRIWA NA MAHAKAMA KUJA KUJIBU KESI YA MADAI NO. 5/2023** DHIDI YA **ANTONY EXPEDITO LWIMBO** kwa hiyo unatakiwa kuhudhuriwa binafsi katika Mahakama hii tarehe 01 Mwezi 06 Mwaka 2023 saa 8:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15 Mwezi 05 Mwaka 2023.

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZINIA**

**Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai Na. 120/2023**

**JINA LA MDAI....................IMARISHA MAISHA FINANCIAL LTD**

**JINA LA MDAIWA............................AUGUST JOSEPH SHAO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA; MTILIGA NDIMI MUSSA - DODOMA MJINI**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TSH. 1,659,140.63**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29/05/2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15 Mwezi 05 Mwaka 2023.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZINIA**

**Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai Na. 140/2023**

**JINA LA MDAI..........................IMARISHA MAISHA FINANCIAL**

**JINA LA MDAIWA............................HUSSEIN COSTA MORIS**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA; HUSSEIN COSTA MORIS**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA 1,145,335.95 TSH.**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 15/06/2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini . Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 22 Mwezi 05 Mwaka 2023.

# Zitto alia na uzalishaji wa makaa ya mawe

**Na Julieth Mkireri,**
SONGEA

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema serikali inatakiwa kuangalia uwezekano wa haraka wa kutengeneza reli ya kutoka Mtwara-Mbambabey kwenda Mchuchuma na Liganga kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe.

Amesema hatua hiyo itaokoa uharibifu wa barabara na kutoa usafiri nafuu kwa makaa ya mawe yanayotoka Mbinga na Peramiho.

Aliyasema hayo jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika Soko Kuu la Songea, akisema magari yanayobeba makaa ya mawe kutoka Songea kwenda Bandari ya Mtwara yanachangia uharibifu wa barabara hiyo.

Zitto alisema magari 1,300 yanadaiwa kutoka na kuingia kila siku Songea huku wakazi wa Mkoa wa Ruvuma wakiwa hawafaidiki na makaa hayo yanayosafirishwa.

"Pendekezo letu katika eneo hili ni reli hii itengenezwe kwa haraka kuleta unafuu kwa wasafirishaji na pia barabara hizi zisiharibiwe" alisema.

Pia alisema chama hicho kinataka kuona makaa ya mawe yanawanufaisha wakazi wa Mkoa wa Ruvuma kutokana na mchango wake kwa sasa katika kuingizia nchi mapato ya fedha za kigeni.

"Uzalishaji wa makaa ya mawe kutoka Mkoa wa Ruvuma kwenda nje ya nchi umefikia dola za Marekani milioni 225 kutoka dola za kimarekani milion 31 kwa mwaka 2022 ambazo zinachangia fedha za kigeni hapa nchini kuliko ilivyokuwa kwa korosho, pamba na kahawa" alisema Zitto

Kwa mujibu wa Zitto, fedha hizo za kigeni zinasaidia nchi katika kipindi hiki cha mtikisiko wa vita ya Ukraine lakini watu wa Mkoa wa Ruvuma hawafaidiki na utajiri huo huku barabara zikiendelea kuharibiwa kila siku na magari hayo.

Hivyo, aliishauri Halmashauri ya Mkoa wa Ruvuma yanapochimbwa makaa hayo ya mawe kukutana na kampuni zinazohusika na uchimbaji kuona namna ya kutengeneza mji kwa ajili ya wafanyakazi ili kuwa na mzunguko wa fedha na kuleta mabadiliko kwenye maeneo husika.

Zitto alisema chama hicho kinahitaji Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi wa kodi za huduma za kampuni zinazojihusisha na uchimabji wa makaa ya mawe.

Alisema ukaguzi huo unatakiwa kufanyika kwenye halmashauri husika kwani zipo kampuni zimekuwa na utaratibu wa kulipa kodi hizo makao makuu ya kampuni zao badala ya halmashauri wanakozalishia makaa ya mawe

Mwenyekiti wa Songea Mjini, Twaib Komba alieleza katika mkutano huo kuwa wakulima wengi hawaridhishwi na uuzaji wa mazao yao kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.




Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyewahi kuwa Mbunge wa Butiama (CCM), Nimrod Mkono baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), jijini Dar es Salaam jana na kupelekwa nyumbani kwake Masaki kwa shughuli za mazishi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# H/shauri yakumbwa uhaba wa walimu msingi, sekondari

**Na Steve Chindiye,**
TUNDURU

HALMASHAURI ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma ina upungufu wa walimu 1,057 katika shule za sekondani na msingi.

Taarifa hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Hairu Hemedi, akisisitiza kuwa hali hiyo imetajwa kuwa kikwazo cha ufaulu kwa wanafunzi.

Akifafanua zaidi kuhusu taarifa hiyo, Mussa alisema kuwa hadi kufikia Machi mwaka huu baada ya shule tatu mpya kufunguliwa, wilaya sasa imefikisha shule 29 za sekondari na za msingi 153.

Mussa alieleza kuwa takwimu zinaonesha kuwa upande wa shule za sekondari kuna upungufu wa walimu 114 wa masomo ya sayansi na shule za msingi kuna upungufu wa walimu 943.

Akitoa ufafanuzi wa suala hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashsuri ya Wilaya ya Tunduru, Chiza Marando alisema kulingana na maelekezo ya serikali, ofisi yake inatarajia kupokea walimu wapya kupitia ajira ambazo zimekuwa zikitangazwa mara kwa mara.

Kuhusu miundombinu ya kufundishia, Marando alisema kwa sasa serikali inaendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya kufundishia katika shue za sekondari na msingi.

Marando alisema halmashsuri imepokea Sh. bilioni 1.176 kwa ajili ya ujenzi wa mdarasa huku Shule ya Sekondari ya Wasichana Masonya ikitengewa Sh. milioni 77. Pia alisema zimetengewa Sh. milioni 410 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika shule hiyo. Shule ya Sekondari Mataka na Mchoteka zimepangiwa Sh. milioni 80 kila moja pamoja na Shule ya Sekondari Nandembo iliyotengewa Sh. milioni 160 kwa ajili ya ujenzi huo.

Akizungumzia uboreshaji wa miundombinu katika shule za msingi, kiongozi huyo alisema kwa sasa halmashauri yake iko katika utekelezaji wa ujenzi wa madarasa 32 baada ya kupokea Sh. bilioni 1.2 kutoka serikalini. Alisema kuwa Shule ya Msingi Mkasale inajengewa madaarasa mawili na matundu ya vyoo matatu yatakayogharimu Sh. milioni 53, Shule ya Msingi Mchangani madarasa mawili yaliyotengewa Sh. milioni 66.3.

Kwa mujibu wa Marando, shule zingine ni Mnazi mmoja inayojengewa madarasa mawili na matundu ya vyoo matatu kwa Sh. milioni 53, Shule ya Msingi Mtina madarasa matano na matundu sita ya vyoo kwa Sh. milioni 130.

Alisema Shule ya Msingi Tinginya inajengewa mkondo mmoja wa madarasa saba kwa Sh. milioni 331 na Shule ya Msingi Mapinduzi itakayojengewa madarasa matatu na matundu matatu ya vyoo kwa Sh. milioni 77.

# DCEA, TAKUKURU waingia makubaliano kushirikiana

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wamesaini hati ya Makubaliano ya Ushirikiano ya kuzuia vitendo vya rushwa na dawa za kulevya kupitia klabu za shule za msingi, sekondari na vyuo.

Makubalianao hayo yalitiwa saini na Mkurugenzi wa TAKUKURU, Salum Hamduni na Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, jijini Dar es Salaam jana.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutia saini makubaliano hayo, Hamduni alisema DCEA na TAKUKURU wamekubaliana kutumia rasilimali walizonazo kuwahamasisha wanafunzi, vijana na jamii kutoshiriki katika vitendo vya rushwa na biashara haramu ya dawa za kulevya na kuchukua hatua stahiki za kukabiliana na mambo hayo.

"Tuna matarajio makubwa baaada ya kutia saini makubaliano haya kwani nguvu yetu ya kudhibiti dawa za kulevya na rushwa itaongezeka na kufanya jamii ya watanzania kuwa salama," alisema Hamduni. Aliwataka wanahabari kutumia taaluma yao kuunga mkono juhudi hizo kwa kuwahamasisha wananchi kushiriki katika kutokomeza vitendo vya rushwa na matumizi ya dawa za kulevya. Kamishna Jenerali wa DCEA, Lyimo alisema: "Nina furaha kutia saini makubaliano haya. Yanaunganisha TAKUKURU na DCEA katika kushirikiana kikazi kutoa elimu shuleni na jamii kwa ujumla juu ya madhara ya dawa za kulevya na rushwa kwa jamii kwa kuwa makosa haya yana uhusiano wa karibu na yanahitaji suluhu ya pamoja."

Alisema muungano huo ni muhimu kwa kuwa utasaidia kufanya matumizi sahihi ya rasilimali chache walizonazo katika kutatua matatizo mawili kwa pamoja.

Pia alisema makosa yanayoshughulikiwa na taasisi hizo mbili ni makosa yenye upinzani katika jamii kwa kuwa yanaleta faida kwa wanaoyafanya.

Alisema kupitia ushirikiano huo na elimu itakayotolewa, vijana watajengewa hali ya uzalendo na kuijenga jamii kuchukia matendo ya rushwa na dawa za kulevya, hivyo kuibua chachu ya maendeleo kwa taifa.

"Rais Samia Suluhu Hassan ana dhamira ya dhati ya kuongoza jamii isiyo na rushwa wala dawa za kulevya. Kupitia makubaliano yaliyofanyika, yataleta tija kwa jamii na kutimiza dhamira ya kuwa na jamii bora ya wachapakazi, jamii ya wazalendo na kulisukuma taifa mbele kupata maendeleo," alisema.

HABARI KITAIFA

# Tanzania kufanya utafiti maeneo yanayoathiriwa na bangi, mirungi

**Na Zanura Mollel**

KAMISHNA wa Kinga na Tiba Mamlaka ya Kuthibiti Dawa za Kulevya nchini, Dk. Peter Mfisi, amesema serikali imeanza kufanya utafiti dhidi ya mazao mbadala kwa wakulima katika maeneo yaliyoathiriwa na kilimo cha bangi na mirungi ikiwa ni mkakati wa kupunguza uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, kiongozi huyo alisema kwa mwaka 2021 na 2022 waliteketeza (kuchoma) kilogramu 100 za bangi zilizokamatwa maeneo mbalimbali nchini.

Alisema kuwa baada ya serikali kubaini wakulima wa bangi na mirungi nchini hufanya kilimo hicho kama zao la biashara, wamejipanga kutoa mbegu kwa wakulima hao ili waachane na biashara hiyo haramu ambayo athari zake ni kubwa zaidi katika jamii.

"Serikali imejipanga kuwapatia ruzuku mbalimbali ikiwamo dawa na kuwatafutia soko la uhakika, zao ambalo tumelifikiria kwa haraka ni pareto ambayo imebanika kuwa na bei nzuri na mkulima atanufaika na kilimo hicho.

"Bangi inastawi takribani mikoa yote nchini, mikoa inayostawisha kama zao la biashara ni Arusha, Morogoro, Mara, Iringa na Njombe. Kwa upande wa mirungi, Same mkoani Kilimanjaro inalimwa kwa makusudi kutokana na soko kupatikana Kenya," alisema.

Dk. Mfisi alisema wamefanya operesheni mbalimbali katika Mkoa wa Arusha ambako eneo la Kisimiri wameteketeza kwa moto mashamba yaliyolimwa bangi, kuchoma zilizovunwa na kuwakamata wakulima hao ikiwa ni sehemu ya kuwachukulia hatua za kisheria.

"Tulienda Same, tumekata mirungi iliyokuwa imelimwa, shida yake ukikata inachipua tena. Huko wanalima makusudi kwa sababu ya kuuza Kenya.

Kuna maeneo mengine mirungi huota kama uoto wa asili. Mfano maeneo ya milimani kama Mlima Monduli na Meru huku Mkoa wa Arusha," alifafanua.

Alisema jitihada za serikali ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuepuka matumizi ya dawa za kulevya ikiwamo mirungi ambayo athari zake ni kubwa. Alitoa mafno kupunguza nguvu za kiume, kukosa usingizi pamoja na kuharibu mfumo wa fahamu.

Alisema nchi nyingi zenye usambazaji na utumiaji mkubwa wa dawa hizo hazina amani, akiitolea mfano Somalia.

Dk. Mfisi alisema Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015, imekataza kumtumia mtu kusafirisha au kusambaza dawa hizo, alitoa rai kwa wote wanaowatumia wanawake na watoto katika shughuli hizo, kuacha mara moja kwa kuwa adhabu yake ni kuanzia kifungo cha miaka 30 jela au maisha.

"Serikali imejenga vituo 15 maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kutolea huduma kwa waraibu wa dawa za kulevyia na hadi sasa kuna watu 15,400 walioathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya ikiwamo heroin, wanaendelea kupatiwa matibabu katika vituo hivyo.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Moshi Kakoso (kushoto), akipata elimu ya matumizi sahihi ya mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa hali ya barabara kutoka kwa Mhandisi Jacob Mukasa wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Muhimbili yakabidhiwa vifaa vya milioni 16.5/-

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Sukos Kova kwa kushirikiana na Peaceland ya nchini China, imekabidhi vifaa vya dharura 15 mahususi kwa kupima kiwango cha oksijeni mwilini vyenye thamani ya Sh. milioni 16.5.

Vifaa hivyo 15 vimekabidhiwa kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ikipokea tisa, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) vitatu na Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) vitatu pia.

Akizungumza baada ya kukabidhi vifaa hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Suleiman Kova, alisema hospitali hiyo na taasisi hizo ni miongoni mwa zinazotoa huduma kitaifa, hivyo zinahitaji vifaa vya kutosha ambavyo vinaokoa maisha ya wagonjwa kila siku.

"Tumejikita katika kutoa vifaa vya msaada kwenye hospitali, shule ili kuwasaidia waathiriwa wa majanga na pia tunatoa elimu kwa jamii kujikinga, kupunguza athari za majanga," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, alisema hospitali hiyo inatumia mitungi ya gesi kati ya 80 na 120 kwa siku, huku uzoefu wa taasisi nyingine JKCI na MOI, wakitumia mitungi 40 kwa siku.

"Vifaa hivi vitatusaidia MNH hasa kwa magari ya kwa ajili ya wagonjwa na wakiona oksijeni ipo chini kwa mgonjwa, watamwekea mgonjwa wakati akiletwa MNH.

"Oxygen concentrator'hii pia inasaidia mazingira hayo. Mfano MNH kuanzia wiki iliyopita tunatoa huduma sio lazma uje hospitali hasa wagonjwa wa muda mrefu, tutakuletea timu nyumbani na pia tunaweza kuja na kifaa hiki," alisema Prof. Janabi.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema wakati kukiwa na ongezeko la magonjwa ya mfumo wa upumuaji hivi sasa, vifaa hivyo ni muhimu hata kuwafikia wagonjwa pale walipo, ikiwamo majumbani.

# Miongozo ya utoaji huduma, malezi kwa watoto yazinduliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua miongozo na nyaraka za elimu ya awali zitakazorahisisha utoaji wa huduma stahiki kwa watoto katika malezi na ujifunzaji ili kujenga makuzi timilifu.

Uzinduzi huo ulifanywa jana na Mkurugenzi Msaidizi Ithibati Shule, Patrick Leyana kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda katika Shule ya Msingi Mtemi Mazengo jijini hapa.

Alisema miongozo na nyaraka hizo zimeandaliwa ili kuwawezesha wadau wa elimu ya awali kutoa huduma kwa watoto wote kwa usawa na kwa kuzingatia mahitaji yao.

Alitaja miongozo hiyo kuwa ni pamoja na Mwongozo wa Kitaifa wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali (MUVEA), Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali (KUMUVEA).

Mingine ni Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji na Utekelezaji wa Shughuli za Ushirikiano wa Wazazi na Walimu katika Elimu ya Awali na Msingi.

Alitaka mwingine ni Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo Shikizi vya Shule pamoja na Mwongozo wa Upimaji Shirikishi wa Matokeo ya Ujifunzaji kwa Wathibiti Ubora wa Shule.

"Shukrani za pekee kwa Shirika la Kimataifa la Watoto Duniani (UNICEF) na GPE LANES II pamoja na mashirika mengine likiwemo shikrika la Children in Crossfire Watoto wetu Tunu Yetu, USAID- Jifunze Uelewe na UKaid-Shule Bora mliochangia kwa moyo wa dhati kufanikisha uandaaji, uchapaji na uzinduzi wa miongozo hii,"alisema.

Hivyo, aliwaomba viongozi wengine kutoka katika wizara zinazohusika na masuala ya watoto kutumia miongozo hiyo ili kuwezesha upatikanaji wa huduma jumuishi kwa watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalumu kufikia viwango vya ubora wa kitaifa, kikanda na kimataifa.

Naye, Mkurugenzi wa Elimu ya Awali na Msingi kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Susan Nussu, alisema miongozo hiyo itasaidia kujenga elimu bora kwa watoto wa kitanzania wakiwa na umri mdogo.

Alisema kupitia mradi wa BOOST walimu 3,000 watafikiwa kujengewa uwezo wa kufundisha madarasa ya awali.

Mratibu wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Hawa Selemani, alisema miongozo hiyo itaweka viwango vya ubora katika utekelezaji wa elimu ya awali.

Mtaalamu wa masuala ya elimu kutoka Shirika la UNICEF, Audax Tibubinda, alisema hatua hiyo inaonesha hatua kubwa katika maendeleo ya elimu na kuhimiza wataalamu wa ndani waendelee kutumika zaidi ili kuleta mafanikio ya aina hiyo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua stahiki zichukuliwe kulinda ikolojia ya Saadani

**UHAI** wa Hifadhi ya Taifa Saadani (SANAPA) uko shakani. Watendaji wa serikali wameimega kwa kutoa vipande vyake kwa kampuni zilizothibitika kuwa na mwelekeo wa kuharibu mifumo yake ya ikolojia.

Hii ni mbuga ya taifa. Lakini kampuni ya kuchimba chumvi - Sea Salt Limited imemegewa kipande. Kampuni ya kuzalisha sukari - Bagamoyo Sugar Limited imemegewa pia. Mmegaji ni yuleyule - serikali ambayo ni mmiliki wa Mbuga ya Saadani.

Tayari Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ameshabainisha hatari inayoikabili SANAPA. Mbuga hii haipaswi kuwa na mwingiliano wa shughuli zozote za binadamu kama uzalishaji chumvi au sukari.

Ni uamuzi sahihi tu unaohitajika kwa kuwa sheria zilishatumika vibaya, ama kwa kutojua au kwa makusudi. CAG anasema shughuli za uchimbaji madini husababisha uchafuzi wa mazingira utokanao na kumwagika kwa mafuta yanayotumika kwenye mitambo, takaoevu, uchomaji taka ngumu, na kelele ndani ya hifadhi.

Bila kuzidhibiti, shughuli hizi zitahatarisha mfumo wa ikolojia ndani ya hifadhi na hivyo kusababisha kutokuwapo uhakika wa uendelevu wake.

Nipashe, tukiwa wadau wakubwa wa utalii na uhifadhi, tunaona kuna haja mamlaka husika kwa maana ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na mamlaka zingine za serikali kuchukua hatua stahiki kuulinda mfumo wa ikolojia wa Hifadhi ya Saadani.

Hifadhi hii ina aina 60 za wanyama. Kuna nyani 2,170, nyati 928, turo 730, twiga 654 na tembo 359 kwa mujibu wa Sensa ya Wanyamapori ya mwaka jana.

Kuna aina zaidi ya 270 za ndege wakiwamo ndege adimu wanaoitwa Sokoke Pipit, wenye rangi mchanganyiko na ambao hawapatikani sehemu nyingi duniani; na kuna mijusi, kenge na mamba katika mfumo wake.

Hifadhi imebeba pia samaki, matumbawe - "vichaka-bahari" chini ya maji - ambako samaki hutaga mayai. Kwenye ufukwe wa hifadhi hii ndiko kwenye mchanga unaoitwa "mchanga wa fungani" - ule uachwapo maji yanapokupwa na ambamo kasa wa kijani hufukua na kutaga.

Saadani pia ina misitu minene ya ukanda wa pwani (Zaraninge); ina makundi ya tembo, nyati, pundamilia, swala na simba; ina utalii wa fukwe na utalii wa boti ili kuona mamba na viboko.

Uzuri na ubora wa Saadani siyo tu wanyama, wadudu na mandhari. Kuna mapato - uchumi. Mwaka 2021/22 peke yake, taifa liliingiza Sh. bilioni moja kutokana na watalii 28,355 waliotembelea mbuga hii.

Yanayoendelea Saadani hivi sasa yanahatarisha uhifadhi na uchumi. Na Saadani ni mali, ni fedha, ni ajira, ni kiburudisho kwa watu wa ndani na nje ya nchi.

Hayo yataendelea iwapo mbuga haitavurugwa kwa kuharibu ikolojia yake na kukatisha uhai wa mimea na wanyama ambavyo ni sehemu kubwa ya uasilli na utajiri wake.


Kunusuru Saadani ni kuacha kutupa chochote mbugani ambacho hakikuwamo; kuondoa mifugo mbugani ili kuepusha mifugo kuambukizwa au kuambukiza magongwa kwa wanyamapori, kupunguza au kuondoa kabisa kelele za binadamu na shughuli hasi kwa uasilia wa hifadhi; na kutoongeza au kupunguza mimea - miti hata maua ndani ya hifadhi.

Kwa hiyo, Nipashe tunashauri mamlaka husika zizuie kukata miti hifadhini, kujenga kiwanda hifadhini kwa ajili ya kuzalisha chumvi na sukari, kubakiza kijiji cha watu wapatao 1,500 ndani ya hifadhi, ambao wataongezeka na hatimaye kuhitaji shule, zahanati na huduma nyingine za msingi. Vitendo hivi vitaua mbuga na uasili wake.

Kinachoendelea Saadani kwa sasa kinakinzana na sheria za hifadhi nchini, na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), ambao pamoja mambo na mengine, unalenga kuimarisha vivutio vya utalii ili vichangie zaidi katika Pato la Taifa na kutoa fursa za ajira. Mamlaka zichukue hatua stahiki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Augusta Njoji

# Ukame unaogonga hodi kitaifa uundiwe mkakati kuepuka madhara

**OKTOBA** mwaka jana haikuwa rahisi kwangu kuamini nilichokishuhudia wilayani Monduli mkoani Arusha, wakazi wake walipolazimika kuweka majivu katika tope ili wapate maji kwa ajili ya kunywa, kupikia na matumizi mengineyo.

Ni kama walikuwa wanakunywa tope, hayakuwa maji tena. Kilifika kipindi walipochota na kujaribu kuweka majivu ili yafae kwa matumizi, hayakufaa tena.

Tope lilikuwa zito kupita kiasi. Hawakuwa na namna. Waliyatumia hivyohivyo. Hasa wananchi wa Kijiji cha Nanja, Kata ya lepruko wilayani Monduli, kulikokuwa na hali mbaya zaidi.

Kwa miaka yote wamekuwa wakitegemea maji kutoka katika mabwawa ambayo hutumiwa na watu na wanyama lakini kutokana na kukosekana kwa mvua ya kutosha, yalikauka na hivyo kusababisha shida hiyo.

Mbali na maji hayo kuwa na tope, upatikanaji wake uligeuka kuwa mgumu na wakati mwingine kulazimika kukesha au kutumia usiku wa manane kuyatafuta.

Maji waliyoyapata mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka jana kutoka katika vyanzo vyao vya mabwawa, yalitoa harufu. Kama una kinyaa huwezi kuyanywa.

Katika hatua zake za awali, serikali iliweka utaratibu wa kugawa walau ndoo moja ya maji (lita 20) kwa kila kaya kila siku hadi pale mvua iliponyesha Novemba mwaka jana.

Kimsingi, kilichoshuhudiwa wilayani Monduli kiliyakumba maeneo mengi nchini kutokana na ukame, japo maeneo mengine hayakufikia hatua ya serikali kugawa ndoo ya maji kwa kila kaya. Ni adha iliyochagizwa na mabadiliko ya tabianchi.

Maeneo mengi nchini mwishoni mwa mwaka jana kuliripotiwa mifugo kukosa malisho na maji huku baadhi ya halmashauri zikilazimika kupatiwa chakula cha dharura kutokana na upungufu wa chakula.

Halmashauri ya Wilaya ya Monduli ndiyo iliyokuwa na madhara zaidi katika upatikanaji wa maji, hata ikifikia hatua hiyo ya serikali kugawa walau lita 20 za maji ya kunywa kwa kaya kila siku.

Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Neville Msaki alisema katika tathmini yao walibaini vijiji vinane wilayani humo viliathirika zaidi, akifafanua kuwa waliomba fedha serikali kuu na kupatiwa Sh. milioni 100 kutekeleza mpango huo wa dharura kwa mwezi mmoja.

Si hayo tu, Oktoba mwaka jana kulikuwa na ripoti ya hali ngumu ya kimaisha iliyowakabili wakazi wa Mtera mkoani Dodoma kutokana na uhaba wa samaki kwenye Bwawa la Mtera linalotegemewa kiuchumi na wakazi wengi wa eneo hilo.

Shida kuu iliyotajwa ni mabadiliko ya tabianchi, wavuvi wengi wakilazimika kuzikimbia familia zao kwenda kutafuta samaki mikoa ya Singida na Tabora.

Mkurugenzi wa Uvuvi, Emmanuel Bulayi, katika ufafanuzi mahsusi kuhusu suala hilo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, aliyataja mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira ni mzizi wa madhara yanayoshuhudiwa kwenye Bwawa la Mtera.

Alifafanua kuwa kupungua kwa maji kwenye bwawa hilo kumekotokana na upungufu wa kiasi cha maji yanayoingia kutoka mito ya Great Ruaha, Little Ruaha na Kisigo kutokana na uharibifu wa mazingira ya vyanzo hivyo na mabadiliko ya tabianchi.

Alibainisha kuwa bwawa hilo lina ukubwa wa kilomita za mraba 660 na wastani wa kina cha maji cha mita 6.2, likipatikana wa ya Dodoma na Iringa.

Kukiwa na madhara hayo yaliyoshuhudiwa mwaka jana, ripoti mbalimbali zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) hivi karibuni, zinaonyesha uwezekano wa kuwapo ukame katika maeneo mengi nchini, hivyo kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi, zikiwamo kilimo na ufugaji.

Kwa kuzingatia uzoefu huo wa mwaka jana na taarifa za TMA, kuna haja kuchukua hatua kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchini kwa kuepuka vichocheo vyake ambavyo ni pamoja na uharibifu wa mazingira na matumizi ya nishati chafu.

MAKALA MAALUM

# Milioni tano za Samia zinavyogeuza soka kuwa ukanda mpya wa uchumi

## -Pia zimo mtaji Uwanja Mkapa, AFCON, ligi nchini ...

Na Mwandishi Wetu

KWA Watanzania wapenzi na wasio wapenzi wa mchezo wa soka wako katika shauku kushuhudia timu yao inavyonyakua ubingwa wa Kombe la Shirikisho la Afrika kuanzia nyumbani Yanga ikimkaribisha mgeni wake kutoka Algeria.

Ni jambo la kihistoria kwani imetimu miaka 30 sasa tangu kuwapo ushuhuda huo nchini, Simba ikikosa kikombe hicho mikononi mwa Stella Abijan ya Misri, taifa likiwa katika zama awamu ya pili ya uongozi.

Pengine inaweza kuwa si sahihi kuoanisha moja kwa moja na wakati ule, lakini kuna yanayoshabihiana. Kwanza timu hizo watani wa jadi, Simba ikiwa katika michuano inayofanana ngazi ya Afrika, ikakwama robo fainali.

Yanga ambayo imekuwa ikipewa jina na Simba wakiitwa 'wa hapa hapa' sasa 'wamepindua meza' ndio inayosonga fainali. Hata utani huo ukashuhdiwa fainali ya mwaka 1993, Simba ilipong'olewa mashabiki Yanga wakiwapa 'kijembe' kuwa "uzalendo (kuwashangilia kama walivyoombwa) umetushinda."

Kwa ujumla ni aina ya mustakabali unaoleta mvutano mkali wa soka, kuanzia nchini hata jicho lote kimataifa linaangukia nchini. Ilikofikia sasa kileleleni tangu timu za Kitanzania kufanya vizuri, katika soka hilo ngazi ya Bara Afrika.

Mvutano huo na unaofanana na huo kwenye ligi nchini, kwa sababu ni wa umati na shughuli za kibinadamu inabeba huduma na biashara kitaifa, ikizingatiwa mashuhuda wamo katikia radio na televisheni za 'vibanda umiza' kila kona, stesheni nyingi za FM sasa soko lao kuu limeegemea michezo na hasa soka.

### NAFASI YA RAIS

Safari hiyo ya soka kadri ilivyong'ara, ndio ikamfungua zaidi msimamo wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kinachobeba tafsiri 'Uchumi Michezo.'

Muundo wa vilabu na timu za michezo kwa asilimia kubwa ni ya mamlaka binafsi. Sehemu kubwa na hasa soka, inaangukia kundi la kuajiriwa hali inayoifanya serikali kuanza kutimiza sehemu ya malengo yake kama vile ajira, kukusanya kodi, uwekezaji, biashara na mzunguko wa fedha.

Mwanzo wa uongozi wake mbali na mpira wa miguu wa netiboli pia ukapata uhai, pia hakuwa mbali na soka la wanawake hata likachukua nafasi yake kung'ara.

Nafasi kubwa sasa imechukua sura, pale Rais Dk. Samia alipojikita hasa kuhamasisha Watanzania kushiriki kikamilifu katika michunano hiyo kimataifa ya soka, Simba na Yanga wamekuwa wawakilishi wa nchi. Hatua kubwa ni pale alipotangaza hamasa ya shilingi milioni tano kwa kila bao linalofungwa kwenye michunao hiyo ilipofika ngazi ya juu.



Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa akitoa fedha za hamasa za Rais Samia Suluhu kwa klabu ya Yanga. **PICHA: MTANDAO**

Zao lake si tu kwamba lilikuwa na hamasa ya moja kwa moja kwa vilabu husika; pia hata kwa mashabiki watu wakisafiri hata kutoka mikoa ya mbali kwenda kuishuhudia timu yao mjini Dar es Salaam, kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Benjamin Mkapa na wapo waliosafiri na timu, ugenini inapoenda.

Ni mwenendo huo kukashuhudiwa baadhi ya mashabiki wakitoka nchi za Ulaya, kwenda kushuhudia mechi ya Yanga, hivi karibuni nchini Afrika Kusini.

Sasa hatua inayofika fainali, Rais Dk. Samia akaahidi penye ushindi kutwaa kombe Yanga itapata Sh. milioni 20, huku ikihakikishiwa usafiri wa ndege ya serikali kwenda ugenini kwenye mechi na baadhi ya mashabiki wake, vilevile kuna tiketi ya bure.

### ZAO LAKE

Aina ya uwekezaji anaofanya Rais Dk. Samia, ni namna ya kutumia vyema sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), pia sera yake iliyopitishwa katika uongozi wa awamu ya nne nchini, dhana ambayo hata bungeni imehimizwa na wabunge hivi karibuni.

Ni uhamasishaji kutoka mamlaka ya juu ya umma, unaoendana na kuingiza fedha na hasa Sh. milioni tano na sasa kwenye michuano ya juu ya Afrika, imekuwa na maana kubwa kwenye mzunguko halisi wa fedha kiuchumi nchini.

Ni hali inayochangia uchumi wa nchi kukua, kuanzia na mambo mawili makuu ambayo ni kilio chake Rais Dk. Samia na serikali yake kuwapatia vijana ajira, hali kadhalika serikali kukusanya kodi zaidi.

Wakati michezo inakuwa ikihahakishwa na pandikizo la mtaji wa 'Mama' Rais wa nchi, ikionyesha kumea kwa kiasi kikubwa katika soka la nchini, inakuza biashara kwa kiasi kikubwa.

Sababu kubwa ni kwamba, kukua kwa soka kunaendana na kukua shughuli za kibinandamu chini, ambazo ndani yake zina mahitaji huduma, machache kuyataja ni vyakula na malazi na usafiri.

Hapo kwa maana hiyo, kunazalisha biashara kupitia haja ya kuwapo hoteli na magari, vyote kuhudumia mahitaji muhimu katika kukidhi mahitaji ya matukio ya soka.

Katika uchumi kuna dhana maarufu ya 'multiplier effect' kwa jambo moja linalofanyikia kuchumi, linazalisha mengine kwa kasi kubwa, mathalan mara baada ya kufanyika upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, ghafla kukashuhudiwa kasi ya uwekezaji hoteli na mahitaji muhimu ya kuhudumia wateja wake katika maeneo jirani.

Hali kadhalika, soka ambako Rais kahamisisha kwa kiungo cha PPP, si kwamba anakoma katika ushabiki kwa timu ya Kitanzania, bali inaifanya kuwa eneo la kisekta kuchangia mengi katika tafsiri ya kiuchumi kwa Watanzania.

Vilevile, shilingi milioni tano na ile 20 ya baadaye, imefungua mlango mkubwa katika eneo la uwekezaji katika soka nchini, timu zilizoko zikikua maradufu na kukuza soko lake, kadri uwekezaji unavyokua, ndivyo zinavyotanua.

Ni hali kiuchumi, inayoasimama katika matumizi zaidi ya fedha ambayo 'multiplier effect' yake kunashuhudiwa kuanzia eneo lililoko timu na kila inakoshiriki, mzunguko wa fedha unakuwa mkubwa na kunakua kiuchumi na maendeleo kwa ujumla.

Pia, kunakuwapo mahitaji ya huduma za kibiashara, kama usafiri na hoteli zinakuwa juu, hata inazalisha makusanyo ya kodi serikalini, pia ajira inapaa zaidi.

Mwisho wa yote inarejesha tafsiri "kukua kwa soka kumechangia kukuza uchumi."

Ni hali ambayo nayo inajenga tafsiri ya mapana michezo hiyo nahata mingine raisa anayohamaisisha kama soka la kinamama, mpira wa pete na ngumi, kwa ujumla wake kadri zinavyokua inakuwa mvuto wa kipekee watu wakitaka kuwekeza katika maeneo mbalimbali yanayohusiana nayo.

### DK. SAMIA NA AFCON

Kuonyesha kwamba anamaanisha katika eneo hilo, Rais Dk Samia, juzi kapiga hatua nyingine rasmi pale alipoweka kuridhia michuano ya Soka Afrika (Afcon), mwaka 2027 kufanyika nchini.

Hiyo nayo inabeba maana kubwa, wageni kuja kuweka kambo nchini na kukuza biashara maradufu na mengime mengi ya kiuchumi, makusanyo ya kodi nayo yanapaa.

Katika ulimwengu wa uchumki huria, ujio wa wageni una kawaida ya kuimadi mpja kwa moja soko la vivutio nchini kimataifa, katika fursa za wageni kuja kuwekeza nchini, vilevile kuna ambao watajihusisha moja kwa moja na biashara katika namna tofauti.

Ndani ya hilo, kama inavyojulikana pindi wanavyokuja wageni wa mbali wakiwamo wa kisiasa nchini, huwa na kawaida ya kutumia fursa hiyo kwenye kutembelea vivutio vya kitalii, hata kunaifanya sekta utalii kuwa sehemu ya wanufaika wa soka la nchini.



# Jela miaka 20 kusafirisha dawa za kulevya kilo mbili

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imemhukumu kifungo cha miaka 20 jela, Lione Rayford kwa kosa la kusafirisha kilo 2.188 za dawa za kulevya aina ya heroin.

Rayford alitiwa hatiani juzi mbele ya Jaji Godfrey Isaya baada ya kusikiliza shauri hilo na mahakama kujiridhisha kwamba upande wa Jamhuri umethibitisha shtaka bila kuacha shaka yoyote.

Inadaiwa mtuhumiwa alikamatwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Julai 5, 2018 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) akiwa na kilo 2.188 za dawa ya kulevya aina ya heroin alizoficha katika moja ya mabegi aliyokuwa nayo. Katika shauri hilo, Jamhuri iliwakilishwa na Wakili wa Serikali, Clara Charwe, Erick Shija na Moses Mafuru na walita mashahidi 15.

Upande wa utetezi uliwakilishwa na Wakili Omari Kilwanda ambao ulileta shahidi mmoja na mshtakiwa alijitetea mwenyewe.

Kabla ya mahakama kutoa adhabu, Wakili Moses Mafuru aliwasilisha hoja za upande wa mashtaka za kuomba adhabu kali dhidi ya mtuhumiwa sababu kiasi cha dawa kilikuwa ni kikubwa, hivyo kilikuwa kinakwenda kuharibu na kuathiri sehemu kubwa ya jamii.

Alidai madhara ya dawa za kulevya kama yalivy oelezwa katika taarifa ya Mkemia Mkuu wa Serikali yanasababisha ulevi usioponyeka.

Alidai pia yanasababisha kuharibikiwa na akili na ni dawa ambazo zipo katika kundi la sumu, hivyo athari zake ni mbaya na zenye madhara makubwa kwa afya ya binadamu. Alidai matumizi ya dawa hizo yanaongeza uhalifu kwa maana ya kuongeza vibaka, wezi na hata wauaji, kuharibu akili ya vijana, yanaathiri uwezo wa kufanya uamuzi kuanzia ngazi ya familia, katika ngazi ya uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo wa jamii na katika nchi.

Upande wa mtuhumiwa, ulidai hakuna kumbukumbu za makossa ya nyuma kwa mtuhumiwa, hivyo ni mshtakiwa kwa mara ya kwanza na sheria inaelekeza apewe adhabu ndogo.

Alidai ana familia kwa maana ya mke na watoto wanaomtegemea, hivyo ni busara kupewa adhabu ndogo ili awe na nafasi ya kuendelea kuhudumia familia.

Pia mtuhumiwa ana umri wa miaka 70, hivyo kwa umri wake anastahili kupewa adhabu ndogo hasa ukizingatia umri wake unanyemelewa na maradhi mbalimbali.

Mahakama baada ya kusikiliza maombi hayo ya kupunguziwa adhabu na kupewa adhabu kali ilizingatia hoja zote.

Jaji Isaya alisema: "Mahakama imezingatia maoni ya upande wa mashtaka kuhusu athari za dawa za kulevya kiafya, kijamii, kiuchumi na kimataifa, imezingatia pia kiasi kikubwa cha dawa ambacho mshtakiwa amekutwa nacho na madhara yake ni makubwa kwa sehemu kubwa kwa jamii.

"Mahakama imezingatia pia mtuhumiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza na ana umri mkubwa. Katika kuzingatia maoni ya pande zote mbili Mahakama inatoa adhabu ya kifungo cha miaka 20 gerezani.

"Pamoja na adhabu hii mahakama inatoa amri kwamba vielelezo viharibiwe kwa mujibu wa sheria, hati ya kusafiria zikabidhiwe kwa mamlaka ya uhamiaji kwa taratibu zao.

"Vitu vya mtuhumiwa ikiwamo nguo za kimasai pamoja na fedha ambazo upande wa mashtaka hawakuleta ushahidi kuonyesha kama zilihusika kutenda uhalifu, vyote virudishwe kwa mtuhumiwa," alisema Jaji Isaya.

## Serikali kutilia mkazo katika ufundishaji lugha kimataifa

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, amesema serikali inaendelea kutilia mkazo ufundishaji wa masomo ya lugha za mataifa mengine shuleni.

Alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akipokea msaada ya vitabu 2,700 vya lugha ya kichina kwa ajili ya kufundishia wanafunzi wa shule nchini, ikiwa ni mwendelezo wa misaada inayotolewa na Serikali ya China kwa Tanzania hafla iliyofanyika katika ofisi za ubalozi huo.

"Tunapitia sera ya elimu na moja ya mapendekezo ni kujifunza lugha mbalimbali za mataifa mengine duniani katika shule zetu na tayari tulishaanza kutoa elimu ya lugha ya kichina kwa wanafunzi wetu kwa miaka 16 sasa.

"Tunawashukuru sana wenzetu Serikali ya China kwa msaada na vitabu hivi vitasaidia kuboresha uwiano kati ya wanafunzi na tunawaomba wanafunzi wajifunze kwa weledi mkubwa," alisema Prof. Nombo.

Alisema vitabu 2,700 walivyopokea vitasambazwa kwa shule 18 nchini zinazojifunza lugha ya kichina kwa ajili ya wanafunzi 6,500 wa shule za sekondari wanaojifunza lugha hiyo.

"Leo tumepokea msaada huu ukiwa ni mwedelezo wa ushikiano wetu, walishatoa vitabu vingine, tunaamini vitasaidia kwa kiasi kikubwa wanafunzi wetu kujiendeleza na lugha ya kichina itakayowaongezea ujuzi na ufanisi zaidi," alisema Prof. Nombo.

Alisema mbali na vitabu hivyo pia wanatoa mafunzo kwa walimu wanaofundisha na kusahihisha mitihani ya lugha ya kichina.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, alisema msaada huo wa vitabu waliotoa utasaidia walimu na wanafunzi wengi kuendelea kujifunza historia, tamaduni kuhusu nchi hiyo.



Kamishna wa Ustawi wa Jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Watoto na Makundi Maalum, Dk. Nandela Mhando (wa pili kushoto), akikabidhi cheti cha kufuzu mafunzo ya walezi na wamiliki wa vituo vya kulelea watoto wenye umri wa miaka 2-8 kwa Mwanachama wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Wilaya ya Temeke, Rachel Kabunda mkoani Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vituo Vya Kulelea Watoto Wadogo Dar es Salaam (UVIWADA), Shukuru Mwakasege. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Lumbesa bado tatizo soko la vitunguu Misuna

**Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA**

WAFANYABIASHARA katika Soko Kuu la Vitunguu Misuna Manispaa ya Singida wameendelea kutumia magunia yenye ujazo mkubwa, maarufu lumbesa, kuwanyonya wakulima licha ya serikali kupiga marufuku.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, amesema kuna watendaji katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida wanaonufaika na ujazo wa lumbesa na ndiyo sababu hawataki kudhibiti vitendo hivyo.

Serukamba alisema hayo juzi alipozungumza na wakuu wa wilaya, wakurugenzi, wenyeviti wa halmashauri na watendaji kuhusu ukusanyaji mapato ya halmashauri.

Alisema kuwa alipozuru katika soko hilo, alimwagiza Mkurugenzi wa Manispaa na Mkuu wa Wilaya Singida kuhakikisha watu hawafungi lumbesa, gari lisitoke katika soko hilo kama limefunga lumbesa lakini kinachotokea katika mageti, magari yanakamatwa yamefunga lumbesa.

"Haya magari yanayobeba lumbesa yanapita wapi na DC (Mkuu wa Wilaya) tulikubaliana tuweke geti, lakini ninaona katika jambo hili ni kama kuna watu wanafaidika ,niwaombe wakurugenzi tuwe serious (makini) katika suala la ukusanyaji mapato," aliagiza. Mei 11 mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Serukamba, alipozuru katika soko hilo, alipiga marufuku wafanyabiashara kutumia magunia ya lumbesa kujaza vitunguu.

Pia aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani hapa kuchunguza uhalali wa fedha wanazotozwa wafanyabiashara katika soko hilo. Alitoa agizo hilo baada ya wafanyabiashara kulalamika kutozwa Sh. 200 kwa kila gunia la vitunguu, kila wiki washusha mizigo hutoa Sh. 5, 000, kila gari likiangia sokoni hapo linachajiwa Sh. 10,000 na madalali kutoa Sh. 2,000 lakini fedha zote hizo hakuna stakabadhi inayotolewa.

Serukamba alisema utaratibu ni kwamba kila fedha inayotolewa lazima mtoaji apewe stakabadhi ya malipo, vinginevyo vinapotelea katika mifuko ya watu, hivyo kuwaagiza TAKUKURU kuchunguza na kuchukua hatua za kisheria.

Pia alipiga marufuku wafanyabiashara kutozwa ushuru mara mbili ndani ya mkoa mmoja na kuwataka wakuu wa wilaya kulisimamia kwa kuwa watakaoumia zaidi ni wakulima.

# MAISHA

MEI 28, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili


Ukurasa 14




## JIPAMBE NA SUPU YA MABOGA

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



Rembesha uzio kupendezesha nyumba yako




## KATUNIKA

Ukurasa 16




## Tunaruka hivi na jeans 2023

Ukurasa 13

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | ■ | S | A | U | T | I |
| A | ■ | ■ | ■ | M | ■ | N |
| M | ■ | Z | I | I | ■ | G |
| B | U | U | ■ | M | J | I |
| U | ■ | B | E | I | ■ | Z |
| K | ■ | A | ■ | ■ | ■ | W |
| A | M | A | N | I | ■ | A |


## FUMBO TOTO

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

BAA, SAA, MKE, UZI, KOMWE, INAMA, MTAMA, BISHA, ENDELEA, BURUNDI

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

HAYA WADOGO ZANGU, TUENDELEE NA AMSHA AKILI IITWAYO SUDOKU. JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 2 | 1 |
| | | 4 | |
| 1 | | | 4 |
| 3 | | | |

## WATOTO

# PAKA RANGI



@ A.MSAMBA




KICHEKESHO

MTOTO wa miaka sita alimuuliza babake:

MTOTO: Baba, eti sisi wanadamu tulikuja vipi duniani?

BABA: Mungu alimuumba Nabii Adam na Hawa. Kisha wao wakaanza kuzaa watoto na watoto wakazaa mpaka tukazaliwa sisi. (Mtoto hakuri dhika akamfuta mamake)

MTOTO: Mama, eti sisi wanadamu tulikuja vipi duniani?

MAMA: Wanasayansi wamesema sisi tulitokana na manyani baadae tukawa binadamu. (Mtoto akarudi kwa baba)

MTOTO: Baba mbona mama anasema sisi tulikuwa manyani mwanzo?Au wanidanganya?

BABA: Mwanangu, mimi nimekuelezea kuhusu ukoo wetu. Mamako amekuelezea kuhusu ukoo wao.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Vijue vitu vilivyoiba furaha ya wengi

KARIBU tena msomaji wangu katika duru za Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilijadili kisa kimoja kilichoonyesha sintofahamu katika ndoa moja changa. Ni miongoni mwa vituko vinavyozitesa familia nyingi katika jamii yetu.

Mtu atasema ni afadhali yanayotokea kwake na kwamba eti kwa mwingine yamezidi. Kumbe yote ni maumivu - liwe dogo au kubwa, tayari dosari imeshaingia katika ndoa.

Unaishi na mumeo. Unaona kila kitu ni sawa kumbe tayari yupo adui aliyejificha. Kujua kwamba mambo sasa ni hadharani ni pale utakapoona mambo yanabadilika.

Upendo wa kwanza haupo. Changamko la awali linayeyuka. Vicheko vya pamoja havipo. Ikifikia hapo, ujue tayari ipo shida! Unamsemesha mwenzako anakujibu mkato. Wakati mwingine hakujibu. Anaondoka.

Ni muhimu sana kujua kwamba maisha siyo tambarare vile unavyodhani. Yapo mawimbi na upepo ambavyo lazima vitaleta mitikisiko katika maisha ndani ya familia zetu.

Wiki iliyopita nikasema mama alimwamini sana mumewe akidhani anapokuwa mbali naye hawezi kuwa na uhusiano na mwingine. Kumbe kule anakopelekwa kikazi huwa na mchepuko.

Na hiyo aligundua alipokwenda kumtembelea mumewe aliyepangiwa kazi mkoani. Kwanza alipofika aliona mwonekano wa nyumba ulivyokuwa mzuri, vitu vimepangwa vyema akahisi jambo.

Usiku walipolala, simu ya mume ikaita akapokea na ilikuwa sauti ya mwanamke akimuuliza, mbona leo hukuja kula? Akamjibu nimekula sehemu nyingine. Pia akakatisha mazungumzo akidai analala, hivyo amtafute kesho na kisha kukata simu.

Mama kusikia akajua tayari ndoa imevamiwa. Usiku ule ulikuwa mgumu sana kwake. Japo alikaa siku mbili, nazo zilikuwa ngumu kwani changamko la mume halikuwapo. Akarudi zake ameinamisha kichwa kwa mawazo.

Mwanamke anayepitia mambo ya aina hii na mengineyo, nimwambie hivi; ulimwengu tunaoishi umejaa dhiki na udhia wa kila aina. Upo wakati unaweza kupitia mambo magumu katika maisha yako kiasi cha kupoteza mwelekeo.

Na wakati mwingine ukahisi ni wewe peke yako unayepitia hali ile. Ninataka nikuambie kwamba wewe siyo wa kwanza kupitia hali inayokukumba.

Wapo wengi walipitia mambo magumu na mazito wala hawakumuacha Mungu wala hawakukata tamaa. Walijitia nguvu, wakafuta machozi na kuendelea kusimama. Na mwisho walishinda kwa kishindo! Ushindi siku zote upo mwishoni.

Kabla sijaendelea msomaji wangu, hebu tuelimishane kidogo maana ya kujitia nguvu. Maana ni nyingi lakini hizi hapa chache kukupa mwanga katika maisha yako.

Kujitia nguvu ni kuvaa ujasiri kufanya jambo ulilokusudia. Kuwa na moyo wa uhodari na ushujaa. Kulinda kile ulichokiamini na kukisimamia bila hofu. Kuwa na tumaini kuwa haijalishi ni mazingira gani utapitia lazima utimize kusudi lako.

Maana nyingine ya kujitia nguvu ni ile hali ya kutoogopa japokuwa unapitia nyakati ngumu. Ni hali ya kuendelea japokuwa umefikia mwisho kimawazo na kihisia. Ni hali ya kujitia moyo kuwa jambo fulani litatendeka hata kama mazingira kwa wakati ule yalikuwa siyo rafiki.

Mtu anaweza kujiuliza kwa nini unapaswa kujitia nguvu? Ni muhimu kila mmoja wetu atambue kwamba Mungu anakupenda na amewekeza vitu vingi ndani yako akiamini kuwa utafanikiwa.

Pia anakuthamini na alikuumba kwa namna ya ajabu kama alivyomuumba Adamu na kusema, "ni chema" na ndivyo anavyokuona wewe! Hivyo hupaswi kumvuja moyo maana anakutegemea!

Msomaji wangu, yapo mambo mengine yanakutegemea wewe kuyafanya na siyo mtu mwingine. Upo wakati hupaswi kuwa tegemezi kwa watu wengine.

Kuna wakati utatakiwa kusimama wewe kama wewe kufanya jambo fulani bila msaada wa wengine. Hivyo, kama hutojitia nguvu mwenyewe utashindwa kutimiza kusudi na majukumu yako kama mwanadamu aliyekamilika hapa duniani.

Lingine ni kwamba kama hutojitia nguvu mwenyewe, utajikuta ukiibiwa. Kuvunjika moyo, majuto, kukandamizwa na hofu ni wezi wa hatma! Vitu hivi vinne vimeiba furaha ya watu wengi, vimechelewesha hatma na hata kuangamiza maisha ya wengi!

Vitu hivi vinne vikikushambulia, vitahakikisha vinanyonya nguvu zako zote za kiroho na kimwili. Ili usiwe mwathirika, ni lazima ujitie moyo kwani unapojitia moyo unapata nguvu ya kuvishinda na kusonga mbele kuelekea kwenye hatma yako.

**Msomaji wangu, niishie hapa kwa leo, wiki ijayo tumalizie maana ya kujitia nguvu. Je, una kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Hivi hamkuwaona wakati wanajenga kwenye shoroba?

KAULI ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa ya kuwataka watu wote waliojenga uzio kwenye shoroba za wanyamapori, kuzivunja wenyewe na wale waliohifadhi wanyamapori kwa kuwadhibiti kwa uzio maalum kuwaachia mara moja, inaweza kuwa suluhu ya uvamizi wa shoroba nchini.

Tunampongeza kwa jicho la ziada na maono ya mbali, lakini kwa nini sasa? Hili ndio swali la kujiuliza. Haiingii akilini unawaacha watu wanavamia mapito ya wanyamapori wanajenga makazi ya kudumu, wanajenga 'zoo' na wengine wanajenga vituo vya mafuta na hoteli, halafu ndio serikali inaamka.

Walipata wapi vibali vya ujenzi wa vituo vya mafuta, zoo, hoteli na makazi ya kudumu? Hivi hamkuwaona wakati wanajenga kwenye shoroba?

Uamuzi wa waziri wa kutamka bila kumung'unya maneno, kwamba sheria inamtaka mtu binafsi asihifadhi wanyamapori kwake, una afya kwa ustawi wa wanyamapori na urithi wa Tanzania, kwa vizazi vijavyo.

Hii ni kwa sababu migogoro mingi tunayoisikia kila uchao katika mikoa mbalimbali nchini kati ya binadamu na wanyamapori, inachagizwa na sababu mbalimbali ikiwamo ongezeko la idadi ya watu na shughuli za kiuchumi kwenye maeneo yenye utajiri mkubwa wa ardhi.

Hakuna ubishi kwamba kasi ya wanyamapori kuvamia makazi ya binadamu imeendelea kuwa tatizo siku hadi siku katika ustawi wa jamii, na hakuna anayeweza kukataa mambo hayo yana madhara kwa mazingira na hifadhi za wanyamapori.

Ni dhahiri kwamba shughuli za binadamu zinazofanyika hivi sasa kwenye mapito ya wanyamapori, zinaweka hatari ya kupotea kwa shoroba za asili kutokana na kuongezeka kwa ujenzi wa makazi ya binadamu, hoteli za kitalii, kilimo na huduma za jamii kama afya, shule na miundombinu ya barabara.

Lakini, wakati idadi ya watu ikikua kwa kasi, kuna umuhimu wa kuzifanya hifadhi za taifa, mapori tengefu na mapori ya akiba, kuendelea kuwapo kwa faida za kimazingira ili kulisaidia taifa letu kuiingiza fedha nyingi za kigeni kupitia sekta ya utalii.

Kama ndivyo! Ili kubakiza hai malengo hayo, ni lazima maeneo ya mtawanyiko ama mapitio ya wanyamapori yadhibitiwe kwa namna yoyote ile yasiendelee kuvamiwa ili kuruhusu wanyamapori waendelee kuzaliana na kupata virutubisho ambayo haviko hifadhini.

Shoroba ni eneo linalounganisha maeneo makubwa mawili ya uhifadhi; hifadhi na hifadhi au hifadhi na eneo ambalo wanyamapori hutawanyika kwa nyakati fulani katika majira ya mwaka na baadaye kurejea hifadhini.

Mathalani, uhamaji wa wanyamapori kutoka sehemu moja kwenda nyingine, husaidia kuhamisha vinasaba ambavyo husababisha kuwapo kwa ukuaji mzuri na endelevu na kuondoa uwezekano wa wanyamapori kuzaliana ndugu kwa ndugu, na kisha kudhoofisha ubora wa vinasaba.

Kufa kwa shoroba zetu kutasababisha wanyamapori wanaozaliana kupata vinasaba dhaifu na kuchangia uwezekano wa kutoweka kabisa kwa wanyamapori adimu ambao ni urithi wa dunia.

Shoroba zote zinalindwa na Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009, ambayo imesaidia kupunguza uwindaji haramu na kusambaa kwa magonjwa ya wanyamapori kwenda kwa wanyama wa kufugwa.

Katika muktadha huo, sisi wazalendo na wapenda haki, tunamshauri waziri mwenye dhamana asilizungumze hili kisiasa, bali akitekeleze kisheria kwa kutazama wapi walijikwaa na kuacha majengo hayo kumea na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kwenye shoroba.

Tazama tishio hilo linavyoakisi wanyamapori 3,340 waliovamia makazi katika wilaya 91 kati ya mwaka 2016 na 2019, sawa na watatu waliovamia kila siku kama inavyoelezwa katika Ripoti ya Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Migogoro ya Wanyamapori na Binadamu (HWC) ya 2020/24, uliofanyika chini ya usimamizi wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Bila kujali kama walifanya uharibifu wowote katika kijiji husika, wanyamapori hao wakiwamo tembo, viboko, mamba, fisi, nyati, simba, chui na nyani walionekana zaidi katika Wilaya za Siha, Busega, Tunduru, Itilima, Kilombero, Bunda, Bariadi, Manyoni, Serengeti, Rombo na Kilwa.

**Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# CROWN NA UMALKIA WA BIBI HARUSI





**SIKU** yako ya muhimu kama sendoff au harusi unatakiwa kuwa malkia usichukulie poa hata kidogo. Crown au taji la nywele kichwani linapaswa kuwa jambo muhimu kulifikiria ili kukamilisha umalkia wako. Maandalizi ni muhimu kufanyika mapema sana. Maharusi wengine hujikuta wakivaa crown ilimradi kwa sababu ya kusahau siyo zile ambazo zinaendana na vazi na urembo aliloovaa. Sivyo, unatakiwa kujiandaa kwa kuchagua mapema mtindo wa nywele unaotaka kubana, uchague kulingana na urembo unaovaa, kama vile hereni na bangili.
Muhimu unatakiwa kuzingatia ukivaa taji epuka kuvaa hereni kubwa na urembo mwingine wa kukuchosha ukang'aa sana na kupoteza mvuto.





# MITINDO

Na Mary Geofrey

## Tunaruka hivi na 'jeans' 2023

JEANS haijawahi kumkataa mtu, awe mkubwa au mdogo, wanawake kwa wanaume, vazi hili siyo la kukosa kabatini.

Katika miaka ya karibuni fasheni kubwa iliyobamba ni skin jeans ambayo imevaliwa sana na vijana na mabinti.

Katika kipindi cha mwishoni mwa mwaka jana na mwaka huu, staili mpya ya jeans kubwa na pana chini zimeanza kushika kasi.

Siyo ajabu tena kukuta binti kavaa jeans pana chini au linampasuo mkubwa.

Ni fasheni ambayo imebamba zaidi hadi wasanii wa ndani na nje ya Tanzania ambayo inavutia kwa kweli.

Ukivaa 'jeans' pana na 'top' na raba unabamba hata ukivaa 'jeans' pana na blauzi pana bado unaonekana bomba.


Hivyo siyo vazi la kukosa hasa kwa kijana ambaye hutaki kupitwa na ulimwengu wa fasheni kama tunavyoona kwenye picha hapa.





URembo

Na Mary Geofrey



# Tumia maji na sabuni kubandua kucha bandia

KATIKA urembo ambao huwezi kukosa kwa wanawake wengi hasa miaka ya hivi karibuni ni kucha bandia.

Kucha hizi zinanogesha sana urembo kwa wanawake hasa wale ambao bado wanadai kama wasichana na wanawake wa rika fulani hivi.

Baada ya kucha kubandikwa mara nyingi hutolewa saluni ambako umebandikiwa au sehemu wanazotoa huduma ya kusafisha na kupaka rangi.

Wanawake wengi wanajua kubandika lakini hawajui habari za kutoa kucha na ndio sababu unaweza kukuta mwanamke anatembea na kucha za vidole viwili nyingine zimeng'oka lakini amekosa muda wa kwenda saluni.

Na vitu vinavyotumia muda mrefu unapokwenda saluni au sehemu ya kupaka rangi ni kuondoa kucha na rangi ya zamani.

Wengi hawafahamu kama huduma hii wanaweza kuipata nyumbani wakiamini dawa za kuondoa rangi pekee ndio zinazoweza kuondoa tu kumbe sivyo.

Namna ya kuondoa

Bandika maji ya uvuguvugu kisha weka sabuni ya maji na tumbukiza mikono au miguu yenye kucha bandia.

Tumbukiza bila kutoa kwa dakika 15 ili kucha zilowane na kulegea kwa ajili ya kuachana na kucha yako halisi.

Ukishafikisha dakika hizo tumia mkono au kifaa cha kusafishia kucha kuanza kuondoa kucha hizo sehemu ambako bado zimeshikana.

Hakikisha hausababishi jeraha lolote na baada ya hapo anza kuzisafisha kwa brashi na maji safi.

Kucha zako zitakuwa tayari kwa ajili ya kupakwa rangi nyingine au kubandikwa tena kucha upya.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Jipambe na supu ya maboga

SUPU ni mlo wa stata ambao unakula kabla ya kula chakula kizito au kifungua kinywa. Supu ambazo wengi wamezizoea ni za nyama na samaki.

Leo katika safu ya mapishi tutaelekezana namna ya kuandaa supu ya maboga ambayo wengi tumezoea kuinywa kwenye hoteli ni nadra sana kuikuta nyumbani.

**Mahitaji**

Blue band vijiko vikubwa viwili, maziwa vikombe viwili, royco kijiko kikubwa kimoja hadi viwili, pilipili manga ya unga kijiko cha chai kimoja, chumvi kiasi na maji lita mbili hadi tatu.

Mahitaji mengine ni boga kipande nusu, viazi mviringo viwili, vitunguu viwili, karoti mbili na nyanya mbili

**Namna ya kuandaa**

Menya boga, viazi, karoti, nyanya na kwaruza weka kwenya sufuria kubwa na menya, osha na katakata vitunguu kisha ongeza kwenye mboga.

Ongeza maji na chumvi chemsha mpaka vilainike na pekecha ikiwa jikoni na moto kidogo.

Ongeza blue band, maziwa royco na pilipili manga ukikoroga kwa dakika 5 na onja chumvi na pakua kama supu.





MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## Maua yanayoweza kuongeza hewa safi ndani

**Na Restuta James**

MABADILIKO ya tabianchi na uchafuzi wa hewa unaotokana na moshi wa viwandani pamoja na wa magari ni jambo lisilokwepeka hususani kwa wakazi wa mjini.

Katika makala ya leo, tunakuletea maua yanayoweza 'kusafisha' hewa, rahisi kupatikana na kuyatunza pia.

Katika orodha hii, mengi ya maua haya yanahitaji jua au mwanga mdogo na maji kidogo pia. Kwa wale ambao wanakabiliwa na shida ya maji hawana sababu ya kukosa maua kwenye vibaraza vyao kwa kuwa hayahitaji eneo kubwa wala maji mengi.

Snake plant au ulimi wa mama mkwe

Ulimi wa mama mkwe ni wa muhimu sana kutokana na upekee wake katika kuongeza hewa safi ya oksijeni na kusafisha hewa kwa ujumla.

Wataalam wa mimea wanaeleza kuwa ni ua lenye faida nyingi za kiafya ambalo linaweza kuwekwa katika chumba cha kulala kutokana na uwezo wake wa kubadili hewa ya kabonidayoksaidi kuwa oksjeni nyakati za usiku.

Hii ni tofauti na mimea mingine mingi ambayo nyakati za usiku huzalisha hewa chafu badala ya oksjeni kama inavyofanya mchana.

Wataalam wa mimea wanalitaja kama chujio la hewa ya ndani ya nyumba linaloweza kuimarisha afya ya akili hasa likiwekwa chumbani.

Watu wengi wanapenda kuliweka kibarazani na katika maofisi huwekwa eneo la mapokezi. Wataalam hao wanaeleza kuwa ni zuri sana likiwekwa chooni na vyumbani.





# Rembesha uzio kupendezesha nyumba yako

UZIO ni moja ya sura ambazo hutumika kama urembo wa nyumba kulingana na namna mhusika anavyotaka uwe kwa kutegemea na bajeti au ubunifu unaotumika kuutengeneza.

Kwa ujumla, nyumba inapozungushiwa uzio iwe ni kwa ajili ya ulinzi, usalama, faragha au mwonekano, unasaidia pia kuongeza thamani ya nyumba husika.

Kwa mazingira yetu ya kitanzania, kuna uziio wa aina mbalimbali ukiwamo za matofali, mbao, miti, makuti, chuma, aluminum, wavu na mabati.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Stephen Kennedy, anasema kuna mambo ya kuzingatia kabla ya kuweka uzio wa nyumba yako.

Anasema ni vyema ukaepuka kukurupuka kuchagua uzio kabla hujafahamu gharama za utunzaji wake na kwamba endapo utaamua kimakosa, kuna uwezekano wa kuharibu mwonekano wa sura ya nyumba yako hata kama ni nzuri kiasi gani.

"Kwa mfano unapoweka uzio wa mbao, unatakiwa ujue kwamba unatakiwa kupakwa rangi mara kwa mara na ujue zinaoza pia baadaye. Kwa hiyo zinahitaji maboresho ya kila mara kwa sababu pasipo kufanya hivyo zinaharibika, hivi ni vitu ambavyo unapswa kujua katika kila aina ya uzio unaotaka kuweka," anasema Kennedy.

> **"Anasema ni vyema ukaepuka kukurupuka kuchagua uzio kabla hujafahamu gharama za utunzaji wake na kwamba endapo utaamua kimakosa, kuna uwezekano wa kuharibu mwonekano wa sura ya nyumba yako hata kama ni nzuri kiasi gani.**


Jambo linguine, anasema kabla ya kutengeneza uzio wako unatakiwa ufahamu unatakiwa uwe kwa mtindo gani.

Anashauri kwamba uzio wa kurembesha zaidi katika lango kuu ikiwamo kuweka taa za rangi husaidia kuweka mwonekano mzuri wa ukuta na nyumba kwa ujumla.

Kennedy anashauri kuweka uzio wenye kuleta faragha na wa kuimarisha ulinzi katika nyumba na si bora uzio.

Anasema uzio unaoacha nafasi au matundu katika nyumba hauna faragha na wala hauwezi kukulinda vya kutosha, ila unakupa starehe ya kuangalia kinachoendelea nje ya makazi yako unapokuwa umejipumzisha.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
ALIYEKUGONGA NA KUKIMBIA HAJAKUKOMOA NAKUUGUZA UNIKUMBUKE KUNIPIGIA KURA
NAMUACHA TU ABWABWAJE NITAONGEA NAWE PRAIVETI
MAMBO YA SIASA HAYACHANGANYWI NA MAMBO YA KIFAMILIA UTAGOMBANISHA!
SIASA NA WAKE ZA WENZAKO VICHOCHORONI TUKUTAZAME TU?
GESTI CLOSED!
BAR IMEFUNGWA
WACHA BWANA!
NIKUPE MIWANI?
ACHA WIVU NIKIWA NAFAGIA BARABARANI HAWANITAMANI NAKOGA VUMBI
WAKOGA VUMBI NDIO WAHONGAJI HODARI MUME...
...KINYUNYIZO CHA LEO...
JANA KAKA TUMEPIGA MITUNGI MPAKA MIMI NIMEZIMA NIKAAMKIA MONCHWALI HA HA HAA WENZANGU TAAABAN!
UNGE-ZIKWA MZIMA
ZIRAILI ALISINZIA
KACHOMOA?
NAPATA ZAMBI SIJAMALIZA MCHANGO WA HARUSI HII
AFADHALI WEWE UJAMALIZA, MIMI NIMEZAMIA LAKINI NIMETOKA MTAMU
DUME ZIMA NJIA NZIMA UNAPEPESA MIJICHO HUPITWI NA SKETI FUPI KWA NINI?
UTANIUA NITAVIACHA BILA NDUGU MTAZAMAJI
...MLANGO WA RIZIKI HAUNA KUFULI...

# HABARI KIMATAIFA



Eneo la machimbo ya mafuta la Kingfisher oil karibu na Ziwa Albert katika wilaya ya Kikuube magharibi mwa Uganda. **PICHA: MTANDAO**

# Sudan yatoa wito wa kuwasajili tena wanajeshi na askari wastaafu

**KHARTOUM,** SUDAN

JESHI la Sudan limetoa wito kwa askari wa akiba na wanajeshi waliostaafu kusajiliwa tena ili kuongeza nguvu katika jeshi, hatua iliyo kosolewa vikali na waangalizi wa kusitisha mapigano.

Wito wa wanajeshi kujisajili tena kupitia kambi za jeshi zilizopo karibu yao, ulitolewa juzi, huku ikielezwa kuwa hatua hiyo inalenga kuimarisha jeshi la nchi hiyo katika vita vitakavyoendelea vya kuwania madaraka na wanamgambo wa RSF.

Msemaji wa jeshi nchini humo alisema hatua hiyo ni hiyari kwa wanajeshi . Na kwamba sheria iliyopo ya majeshi ya Sudan inasema, askari wastaafu watasalia kuwa askari wa akiba, hivyo wanastahili kuandikishwa upya.

Wakati tangazo hilo la jeshi linatolewa katika baadhi ya maeneo mapigano ya hapa na pale yaliendelea kushuhudiwa kwa wiki nzima, ingawa waangalizi wa kusitisha mapigano Saudi Arabia na Marekani walisema kulikuwa na uzingatiaji, lakini hatua za jeshi zinaweza kuashiria kuwa linajiandaa na mzozo wa muda mrefu.

Wakazi katika mji mkuu wa Khartoum ambao nao umelengwa na mashambulizi wameendelea kuteseka kutokana na kukosa nishati ya umeme, maji safi, huduma ya afya na mawasiliano.

Pia inabainishwa kuwa nyumba nyingi hasa katika maeneo ya mabwanyenye na maduka ya bidhaa za vyakula, viwanda vya chakula kama unga na mahitaji mengine muhimu kumeshuhudiwa uhalifu wa uporaji.

"Yote ni sehemu ya machafuko ya vita hivi, na hata kama tungelikuwa Sudan, hakuna unachoweza kufanya" alisema

Taysir Abdelrahim,ambae yupo nje ya nchi amegundua uporaji nyumbani kwake.

Shirika moja linalosaidia watoto walio na saratani lilisema kwamba nyumba ya wageni inayofanyia kazi imevamiwa, ikiwa ni pamoja na vyumba vyake vya usalama na vya wagonjwa.

Naye Kiongozi wa jeshi Abdel al-Burhan, alimwandikia ujumbe Katibu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres jana, akimtaka kumuondoa mjumbe wake Volker Perthes.

Hata hivyo, vyanzo vya ndani ya jeshi havijaeleza kwa undani sababu za hitaji hilo, lakini Perthes, ambaye aliteuliwa 2021, alichangia kusukuma mbele ajenda ya kipindi cha mpito kuelekea utawala wa kiraia, ambao baadhi ya maofisa wa jeshi walipinga mchakato huo.

UN kupitia msemaji wake Stephane Dujarric, alisema, Katibu Mkuu amestushwa na wito huo wa kiongozi wa kijeshi na kwamba Guterres anajivunia mjumbe huyo maalum.

Kwa mujibu wa UN Mapigano hayo yaliozuka mnamo mwezi April yamesababisha takriban watu milioni 1.3 kukimbia makazi yao, takriban 840,000 wakikimbilia katika maeneo salama ndani ya taifa hilo huku wengine wapatao 250,000 wakivuka mipaka na kuingia mataifa jirani.

Katika hatua nyingine Wizara ya Afya ilisema takriban watu 730 wamefariki dunia, ingawa kuna uwezekano mkubwa idadi hiyo ikawa ni kubwa, huku miongoni mwa waliofariki ikiwa ni watoto wadogo na wanawake.

Vile vile, taarifa ya wizara hiyo ilisema nusu ya watu wa Sudan wapatao milioni 49 wanahitaji msaada.

Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) lilisema nafaka za kulisha takriban watu milioni mbili kwa mwezi zitawasili kwa meli ingawaje haikuwekwa bayana ni lini hasa zitawasili.

Pia inaelezwa kuwa bado haijulikani ni kwa namna gani misaada mingine ya kiutu itawafikia wasudani wengine ambao usalama wao sio wa uhakiki.

Saudi Arabia na Marekani zilisema kwamba baadhi ya misaada ilifikishwa Khartoum juzi, huku Msalaba Mwekundu nyao imesema ilifanikiwa kupeleka vifaa katika hospitali saba.

**DW**

## Uganda yakaribia uamuzi uchimbaji mafuta

**KAMPALA,** UGANDA

UGANDA inatarajiwa kufanya uamuzi wa mwisho wa kuchimba na kusafirisha mafuta, baada ya kufikia kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda chake cha kusafisha malighafi hiyo.

Wizara ya nishati ya Uganda, ilisema jana kwamba hatua hiyo inayotarajiwa kufanyika mwezi ujao, ni muhimu wakati nchi hiyo ikijitayarisha kuanza kuchimba mafuta ghafi ifikapo mwaka 2025.

Uganda iligundua kuwa na mafuta katika eneo la Albertine, magharibi mwa nchi, miaka 10 iliyopita, huku ikikadiriwa kwamba kuna hakiba ya mapipa bilioni 6.5 ya mafuta ghafi.

Wizara ya nishati na madini ilisema kwamba mazungumzo yanaendelea na makubaliano yanatarajiwa kufikiwa Juni mwaka huu.

Kampuni kadhaa ikiwemo General Electric, ya Marekani, zinatarajiwa kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta, chenye uwezo wa kusafisha mapipa 60,000 kwa siku, kwa gharama ya kati ya dola bilioni tatu na nne.

Pia ilielezwa kuwa vitalu vingi vya mafuta nchini Uganda vinamilikiwa na kampuni ya Ufaransa ya Total, CNOOC ya China na kampuni ya mafuta ya kitaifa ya Uganda UNOC.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa uchimbaji wa mafuta katika mradi wa Tilenga, huko Ziwa Albert, utaanza mwezi ujao.

**VOA**

# Papa Francis arejea kazini baada ya kuugua

**VATICAN,** ITALIA

KIONGOZI wa kanisa Katoliki duniani Papa Francis (86) amerejea kazini baada ya likizo aliyopewa kutokana na changamoto za kiafya.

Hayo alibainishwa na ofisi ya Vatican, ikieleza kuwa Papa alilazwa hosipitalini kutokana na matatizo ya kupumua miezi miwili iliyopita.

Msemaji wa Vatican Matteo Bruni jana, alisema kuwa raia huyo wa Argentina hangeweza kukutana na watu kama alivyokuwa amepangiwa kutokana na hali ya homa, licha ya kwamba haikuwa wazi ni nani alitarajiwa kukutana na Papa.

Katibu wa mambo ya nje wa Vatican Pietro Parolin, alisema kiongozi huyo huenda amechoka kutokana na mipango mingi kwenye ratiba yake.

Papa Francis alikuwa na mikutano minane Alhamisi, kwa mujibu wa ratiba yake iliyochapishwa mwanzoni mwa wiki hii, na kwamba alipangwa kukutana na Rais wa Italia Sergio Mattarella.

Inaelezwa kuwa Papa Francis, tangu 2013, amekuwa akikabiliwa na changamoto za kiafya, na kwamba amepata matatizo yanayoongezeka ya kiafya na maumivu ya mara kwa mara kwenye goti lake la kulia hadi kulazwa hospitalini hivi karibuni akikabiliwa na matatizo ya kupumua.

Matukio hayo yamezua wasiwasi mkubwa na kuchochea uvumi kwamba anaweza kuchagua kustaafu badala ya kuendelea na kazi kama alivyofanya mtangulizi wake, Benedict XVI.

Mwishoni mwa mwezi Machi, Francis alilazwa hospitalini huko Roma baada ya kuwa na shida ya kupumua, ambapo alikaa kwa siku tatu.

Pia inabainishwa kuwa alipotoka katika hospitali ya Gemelli Aprili mosi, mwaka huu, Papa alitabasamu na kufanya mzaha na watu waliomtakia heri, akicheka na kusema "Bado niko hai!"

**RFI**

HABARI/SAFU



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Henry Mwaibambe akizungumza na wamiliki bodaboda na bajaji na madereva wake, viongozi wa Serikali za mitaa na wa vyama vya waendesha bodaboda kuhusu kujiepusha kushiriki katika vitendo vya uhalifu jijini Tanga juzi. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Watalii toka Italia wamiminika Tanzania

**Na Mary Geofrey**

UBALOZI wa Italia nchini, umesema ushirikiano wa zaidi ya miaka 100 na Tanzania, umesaidia kuwafanya raia wa nchi hiyo kuingia nchini kwa ajili ya utalii.

Kuanzia Januari mwaka huu, Waitaliano 10,338 waliwasili nchini kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Zanzibar kwa ajili ya utalii.

Balozi wa India nchini, Marco Lombardi, alibainisha hayo jana nyumbani kwake, Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa Siku ya Kitaifa ya Italia, maarufu 'Festa Della Repubbica'.

"Shukrani za pekee ziende kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutengeneza filamu ya The Royal Tour ambayo ina mchango mkubwa katika kufufua tasnia ya utalii baada ya janga la UVIKO-19. Kwa hakika ulihitajika msaada wa kiwango cha juu, ameweka wazi vivutio vya kipekee vya nchi hii kubwa," alisema Balozi Lombardi.

Alisema mashirika yasiyo na kiserikali kutoka Italia yanajihusisha na miradi mingi muhimu katika sekta ya afya na kilimo.

Alisema Italia imetia saini makubaliano ya kuwekeza dola za Marekani milioni 20 katika mafunzo ya ufundi na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

"Tunafanya kazi pia kusaidia uwekezaji wa wanawake na vijana katika jamii hii yenye idadi kubwa ya vijana na pia katika kukuza uchumi wa buluu," alisema.

Akizungumzia maadhimisho ya siku hiyo kwa mwaka huu, alisema yataanza Juni 2, ambayo ni Siku ya Taifa la Italia na yatafanyika nyumbani kwa balozi.

Alisema Juni 3, kutakuwa wabunifu na wasanii mbalimbali wa Italia na wa ndani watakaoonyesha bidhaa zao.

"Kwa niaba ya familia yangu, ninawakaribisha nyote kuwa sehemu ya madhimisho ya mwaka huu na mfululizo wa matukio yake. Tunatazamia uhusiano wa muda mrefu wenye manufaa kwa nchi ya Utalia na Tanzania," alisema Balozi Lombardi.

# 15,000 watoa taarifa matatizo wanayokutana nayo barabarani

**Na Neema Emmanuel**

WANANCHI 15,000 wameingia kwenye mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa hali ya barabara na kutoa taarifa ya matatizo wanayokutana nayo pindi wanapotumia barabara.

Kaimu Meneja wa Mfuko wa Barabara, Rashid Kalimbaga aliyasema hayo wakati wa utoaji elimu wa matumizi sahihi ya mfumo huo kwa wabunge katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma.

Alisema tangu kuzinduliwa kwa mfumo huo Julai mwaka jana jijini Mwanza, tayari wamepokea taarifa za hali ya barabara zaidi ya 15,000 na taarifa 9,300 ambazo ni sawa na asilimia 62 ya taarifa zilizotolewa.

"Kwa hiyo, utaona kwamba ni mfumo ambao unafanya kazi, taarifa zinakuja na zinafanyiwa kazi na mwananchi ambaye anatoa taarifa anapatiwa mrejesho kwa wakati kulingana na tatizo aliloliripoti," alisema.

Kalimbaga alisema taarifa hizo zinahusu hali ya barabara kama vile dharura ya kalavati limezolewa na mafuriko ya mvua, barabara imekatika, kuwapo shimo barabarani au alama za barabarani zimeibwa.

Alisema wananchi wanaweza kutoa taarifa ya hali hiyo kupitia simu za mkononi na taarifa hiyo itafika moja kwa moja kwa wakala wa barabara husika na watachukua hatua na kuitolea mrejesho kwa mtoa taarifa.

Alisema kuwa Bodi ya Mfuko wa Barabara imeamua kuweka kambi bungeni ili kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mfumo huo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa hali ya barabara kwa wabunge ili wakiuelewa wasaidie kutoa elimu kwa wananchi katika majimbo yao.

Mhandisi Jacob Mukasa kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara alisema mfumo huo ni rahisi kutumika na kila mwananchi kwa kuwa unapatikana kupitia simu za mkononi.

Alisema mfumo huo uitwao 'barabara' unapatikana kwa kupakua kupitia App Store au Play Store au kwa kubonyeza *152*00# kuchagua namba nne halafu tano na kisha kufuata maelekezo ya kutoa taarifa za hali ya barabara.

Bodi ya Mfuko wa Barabara iliunda mfumo huo kwa kutumia wataalamu wa ndani ili kuwashirikisha wananchi katika ufuatiliaji wa hali ya barabara na hivyo kuongeza ulinzi wa miundombinu ya barabara ambayo serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kuijenga.

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Baba asimulia kisa cha binti yake kutungiwa wimbo 'Afro'*



**Na Adam Fungamwango**

AFRO ooh , Afro mama oh oh, mtoto wa Sagana eeh mama, salamu zangu nakutumia, popote ulipo uzipokee. Nisalimie ndugu na wazazi wako mama eeh popote walipo Afro, mimi sijambo lakini mawazo tele, moyoni nina wasiwasi, nikikumbuka tulivyoachana, mara ya mwisho uliniahidi Afro, tungeonana mapema siku zinapita bibi eeh mbona sikuoni, Afro mama, eeh iya ohoo, mtoto wa Sagana, eeh eeh

kaa ukumbuke, eeh, penzi hugeuka eeh leo kwangu kesho kwako, mama eeh utanikumbuka eeh."

Leo naanza na mashairi wa wimbo huu. Unaitwa 'Afro', ambao kwa kweli ni maarufu si Tanzania tu, bali Afrika Mashariki na Kati.

Hata leo ukipita kwenye bendi mbalimbali zinazofanya muziki wake 'laivu' huwezi kukosa kuusikia wimbo huu wakiupiga 'kopi' au vijana wa sasa wanaita 'cover.'

Ulitungwa na kuimbwa na mwanamuziki John Ngereza na wenzake wa bendi ya Les Wanyika mwanzoni mwa miaka ya 1980.

Ngereza ni mmoja wa Watanzania waliotoka Tanga na kwenda nchini Kenya kufanya kazi ya muziki. Ikumbukwe kuwa Les Wanyika ni bendi iliyoundwa na asilimia zaidi ya 90 na wanamuziki wa Kitanzania, waliojiengua kutoka bendi ya Simba Wanyika, iliyokuwa chini ya Wilson Peter 'Kinyonga' na ndugu yake George Peter. Ndugu hao walijitenga na bendi ya Jamhuri Jazz ya Tanga na kukimbilia nchini Kenya kufanya makazi, wakaunda bendi iliyoitwa Arusha Jazz na baadaye wakaibadilisha jina na kuiita Simba Wanyika.

Baada ya kutamba kwa muda mrefu, baadhi ya wanamuziki wakajitenga na kufanya makazi yao huko huko nchini Kenya, wakaunda Les Wanyika ambalo lilifanya makubwa sana, likitunga na kurekodi vibao vikali kama 'Sina Makosa', 'Paulina', 'Pamela', 'Amigo', 'Nimaru', 'Ufukara si Kilema,' 'Nisaidie', na nyingine nyingi.

Mmoja wa wimbo uliokuwa maarufu ni huu wa 'Afro'. Wengi waliokuwa wakiukia wakati huo kwenye redio, sahani za santuri na mpaka sasa zinapopigwa kwenye kumbi mbalimbali zinaleta bendi za muziki kupiga 'laivu' hawajui ulitungwa vipi na sababu ya kutungwa pia.

Taarifa tu iwafikie kuwa mwanamuziki huyu wa Kitanzania, Ngereza alimtungia mwanadada mmoja mrembo wakati huo aitwaye 'Afro'. Alikuwa ni binti mmoja mrembo aliyeumbwa akaumbika mwenyeji kijiji cha Karima, kilichopo mji wa Sagana, Wilaya ya Kirinyaga, Mkoa wa Kati nchini Kenya.

Uthibitisho wa hili anao baba yake mzazi binti huyo aitwaye Mwangi wa Mburu ambaye alifanyiwa mahojiano na stesheni ya televisheni NTV ya nchini Kenya.

Katika mahojiano hayo yaliyofanyika mwaka 2019, mzee huyo alifichua kuwa kumbe ilikuwa ni hadithi ya kweli, wimbo huo ulimhusu binti yake ambaye alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na mtunzi Ngereza.

"Nilishtuka, akaniambia baba fungua redio utasikia mimi nipo, naimbwa, baadaye nikausikia. Nikamuuliza huyo anayekuimba haja yake hasa nini nini? Akaniambia alimuimba kwa sababu au maana ya mpenzi tu ya vijana. Nikamuuliza kazi yake ni hiyo muziki? Akanijibu ndiyo. Siku moja nikamwambia huyo Ngereza kama anataka kukuoa siyo vema, kwa sababu hawa watu wa muziki ni watu wa raha raha sana, kwa hiyo kama urafiki uwe wa kujishikiza tu sawa, lakini si wa kuolewa," alisema mzee Mwangi.

Mzee akaenda mbali zaidi na kusema kwelie wimbo kuna kipande kinasema atakwenda kwa akawaone wazazi wake huyo binti, lakini hawakwenda wala kuletwa kama ambavyo aliomba kwa binti yake.

"Tena kwenye huo wimbo waliimba tunakwenda kwa baba yako tukasalimie, wala hata hawakuja hapa, wala hawakuletwa." Akasema Mwangi huku akiangua kicheko,"

Kipande cha maneno haya yapo 'korasi' ya wimbo wenyewe ambayo ni haya.

"Afro wa Kirinyaga, Sagana ee, usiniweke pembeni mama, ingawa wako wengi wazuri Mami, lakini nimekuchagua wewe, tabia zako rawa na sura yako, nimeridhika kuwa na wewe, Sagana unipeleke mama ooho, nikawaone wazazi wako mama, na TZ (Tanzania) pia tufike Mami, ukawaone baba na mama eee, mingine mengi sisemi mama aa, uamuzi nakuachia wewe, mwisho namuombea salama Afro, mpaka siku tutapoonana Mami."

Mzee Mwangi mwisho wa yote alisema wimbo huo ulimbeba au kumsaidia binti yake awe ni binti mwenye kupendwa na wengi zaidi kiasi cha kumfanya kupata bwana aliyemuoa na kupata watoto watatu.

"Mwishowe binti yangu akaolewa, tukaacha habari ya kuimbwa kwenye redio na santuri, akapata bwana, nikapewa mahari, nikafurahi, akapata watoto watatu huko alikoolewa." Mzee Mwangi alimalizia stori ya asili ya wimbo wa 'Afro' ambao alitungiwa binti yake mwenyewe, na mpenzi wake Ngereza.

Mzee akawa na wasiwasi na mwanamuziki, akaona akimuoa huenda asimtunze na kumtelekeza binti akateseka kutokana na hisia kuwa wanamuziki ni watu wanaopenda au kupendwa na wanawake wengi, baadaye akaolewa na mwanaume mwingine kabisa. Ngereza alifariki mwaka 2000 nyumbani kwao Tanga.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-12

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

MARA kwa mara alikuwa akimtupia jicho Dan anapotoka kidogo au kurudi ni mwanamke gani anamfuata, au nani anaingia baada ya yeye kurudi ndani.

Akili yake ilimtuma kwa sababu siku ile alijinasibu kuwa familia ya kina Dan inamtambua yeye, basi ni lazima angekuwepo. Na kwa sababu asingeweza kufahamu kama yeye angekuja kwenye pati hiyo, hivyo angefika tu kwa kujipendekeza kwake.

Japo ilikuwa ni pati ndogo tu ya 'bethdei', lakini ilifana. Keki ikakatwa, watu wakaimba.

Wakaila. Wakacheza muziki. Wakala na chakula, kunywa na kufurahi.

Wakati ikielekea kwenye kilele ndipo Belo aliponyanyuka na kutoa risala fupi ya shukrani.

"..Nawashukuru sana wote mlioshiriki kwenye tafrija hii fupi ya 'bethdei' ya binti yangu Tima.

Lakini kwa dhati kabisa napenda kumshukuru mke wangu mama Tima ambaye tumeshirikiana naye sana kwenye hili lililotuleta leo hapa. Mwingine ningependa kumshukuru mdogo wangu wa kuzaliwa tumbo moja, Dan. Yeye pamoja na kwamba alipaswa kusafiri leo hii, lakini ameahirisha kwa sababu ya hafla hii.

Kipekee kabisa kabla sijamaliza ningependa kumshukuru shemeji yangu, Husna na mama yake kwa kukubali ombi langu la kuwaalika na kweli wakatekeleza.

Kukubali ni jambo moja, lakini kufika hapa ni jambo lingine. Kusema kweli haikuwa kazi rahisi kuwashawishi kuja kwenye pati hii. Ilikuwa ni jambo la kujitoa muhanga mimi kwenda kwao na kufanya ushawishi kwa ajili ya hili lililotokea.

Nikisema hivyo nadhani wengi wanajua nini kilitokea huko nyuma, hivyo ilikuwa si rahisi.


Lakini walinikaribisha vema kwao, nikafanya nao majadiliano na kuwaalika hapa na ndiyo maana wamefika.

Kwao ulikuwa ni mualiko maalum." Belo aliongea. Sauti yake ilipenya vema masikioni mwa ndugu yake Dan.

Ndipo alipofunguka masikio kuwa kumbe kaka yake, Belo ndiye aliyekwenda ukweni kuwaalika mkewe na mama mkwe wake.

"Du! Kaka kaingia kwa gia gani?" Akajiuliza. Baada ya kujiuliza sana akajipa jibu mwenyewe na akili yake ikatulia.

"Husna hakugombana na kaka Belo. Mgomvi wake ni mimi, hivyo asingeweza kumtolea maneno ya shombo na kumtimua. Alikaa, akamsikiliza, wakaelewana." Akajibu.




**"Niliporudi kuna vitu nilikuta haviko sawa, kwa hiyo ilibidi mimi mwenyewe nianze kuhaha huku na huko ili kuweka mambo yarudi kama yalivyokuwa mwanzo. Na katika kuweka mambo hayo sawa, katika kuulizauliza, ndipo kuna watu wakanikutanisha na huyu bwana, anaitwa Belo.....**

"Nimshukuru pia mdogo wangu Dan, naye amekuja hapa na amekuwa mtulivu pamoja na mambo kadhaa yaliyopita hapa kati, lakini hayakumchanganya, amekuwa na sisi katika hafla hii muhimu ambayo inawezekana ikawa ya kukumbukwa.

Na pia niwashukuru dada zangu Tunda na Halima, hawa kwa kiasi kikubwa wamefanikisha zaidi kwenye masuala ya vyakula, mmewaona akinamama huko nyuma wakiwa wanatengeneza chakula kizuri ambacho kimetushibisha siku hii ya leo, wao wamefanya kazi kubwa ya kuwaalika mashoga zao ambao wameipata tafrija hii kiasi kwamba hata mimi mwenyewe awali nilitaka iwe ndogo tu, lakini kwa namna ya pekee na ambayo sikutarajia imekuwa kubwa kuliko nilivyodhani.

Ni Mungu tu ndiyo wa kumshukuru." Akamaliza kushukuru Belo.

Wakati kila mmoja akidhani sasa atawaruhusu watu kuondoka, kwani baadhi tayari walikuwa wameshabeba na vinywaji vilivyobaki wakiviweka kwenye mikoba yao.

Sauti ya Belo ilisikika tena. Bado hakuruhusu waalikwa kuondoka.

"Ila siwezi kumaliza kufunga tafrija hii bila kumnyanyua rafiki yangu Massawe. Huyu ni rafiki yangu, lakini hatukufahamiana siku nyingi sana, ni muda mfupi tu. Ana machache ya kutaka kuwaelewa. Karibu sana bwana Massawe."

Alinyanyuka bwana Massawe ambaye hakuwa amekaa mbali sana na Belo.

Alionekana kujiandaa na ilionekana si muongeaji sana kwa watu. Alichukua nusu dakika kujitengeneza, kuweka vizuri shati lake, na kutafuta maneno ya kuongea.

"Nashukuru sana bwana Belo kwa kunipa fursa hii adhimu kwenye hafla hii fupi ya 'bethdei' ya binti yetu Tima anayetimiza miaka 10 leo. Sherehe imekwenda vizuri, hakuna tatizo lolote, watu wamekula, kunywa wakacheza muziki na wengine kufahamiana.

Hata mimi kuna baadhi wameshangaa kuniona hapa leo."

Mmoja wa watu walioshangaa kumuona pale ni Dan.

Anamfahamu Massawe kuwa anaishi maeneo ambayo yeye pia anaishi, Mabibo.

Alishangaa kumuona pale kwenye pati ya kaka yake. Hakutarajia wala kuwaza kuwa kaka yake Belo na Massawe wanafahamiana.

Mwingine ni Husna, mkewe Dan. Kama ilivyo kwa mumewe anamfahamu mtu huyo vizuri tu kwa sababu hawaishi mbali na pia hata eneo ambalo anafanyia shughuli zake ziko kule kule Mabibo.

Leo amemuona Manzese Tip Top na hakuwaza kama ana ukaribu au urafiki na shemeji yake Belo.

Kwa sababu hata hakuwahi kuona ana urafiki na mumewe. Huwa anaongea naye kwa sababu tu ya shughuli anayoifanya.

"Mimi naishi Mabibo. Ni jirani tu na anapoishi Dan, tunafahamiana lakini sio kivile, hata mkewe tunafahamiana lakini sio kwa kiasi kikubwa. Mimi nafahamiana na wengi kwa sababu tu za kibiashara ambayo nitaitaja baadaye.

Hivi mnavyoniona nina wiki mbili tu tangu nimerudi kutoka Moshi, nilifiwa na baba yangu mzazi ndiyo maana sikuonekana kwa mwezi mzima."

Wahudhuriaji wote walikaa kimya wakimsikiliza Massawe ambaye ndiye mtu pekee mpaka sasa aliyepewa nafasi ya kuongea kwenye hafla hiyo ukiacha mwenyewe Belo.

"Niliporudi kuna vitu nilikuta haviko sawa, kwa hiyo ilibidi mimi mwenyewe nianze kuhaha huku na huko ili kuweka mambo yarudi kama yalivyokuwa mwanzo.

Na katika kuweka mambo hayo sawa, katika kuulizauliza, ndipo kuna watu wakanikutanisha na huyu bwana, anaitwa Belo, Ni mtu mzuri, mcheshi, na mpambanaji ambaye kwa ushirikiano wangu mimi na yeye umetufikisha hapa tulipofika.

Kifupi kuna tatizo limejitokeza kwenye biashara yangu. Na sikulijua tatizo hili hadi niliporejea kutoka Moshi.

Na limeleta matatizo makubwa sana na sijui, lakini leo hii hapa nitaweka wazi nini kimetokea na hadi nikaamua kuwasaka wahusika na kwa bahati nzuri nikaangukia kwa Belo ambaye alinipa mbinu hii ambayo tumeifanya kabla watu hawajafahamu lolote na mpaka sasa nadhani imekwenda vizuri.

Basi 'bethdei' ya leo inakwenda kuliweka jambo hili sawa, ili kila mmoja ajue leo nini kilitokea na nini kilifanyika hadi kila kitu kikawa shaghalabagala. Kwanza kabisa niombe samahani kwa sababu chanzo cha yote nitakayoyasema ni mimi hapa."

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# JACKIE CHAN AMTOLEA NJE MWANAYE URITHI


MCHEZA sinema nguli na maarufu duniani, Jackie Chan amesema hatotoa hata senti tano kwa urithi wa kijana wake wa kiume, Jaycee.

Mbabe huyo wa sanaa za mapigano ambaye amejipatia mashabiki wengi duniani, ikiwemo Tanzania kutokana na aina yake ya mapigano, ameshaandika kabisa wosia kuwa utajiri wake unaofikia Dola za Kimarekani milioni 370, sawa na pesa za Kitanzania takriban Sh Bilioni 850, mtoto wake huyo hazimhusu.

Alipokuwa akihojiwa na gazeti na New Asia, Chan alisema ameamua kutompa urithi huo wa utajiri Jaycee mwenye miaka 39 kwa kuwa ana uwezo wa kutafuta, hivyo ni heri akatafuta pesa zake mwenyewe, kuliko kusubiri za urithi atakapokufa.

Mwigizaji huyo kutoka Bara la Asia nchini China amefunguka kuwa sehemu yake ya utajiri itatolewa kwa watu wenye uhitaji, iwapo atafariki dunia.

Jaycee ni mtoto pekee wa Chan kwa mkewe Joan Lin waliyeoana mwaka 1982. Kijana wake huyo ni muigizaji na pia ni mwanamuziki, ambapo mwaka 2014 aliwahi kukamatwa na dawa za kulevya, ikimlazimu Chan kutumia nguvu kubwa kuomba radhi mbele ya umma kuhusiana na hilo.





# Kasambula arejea Bongo

Mwanamuziki mwimbaji wa bendi za zamani za Super Matimila, na Orchetra Safari Sound (OSS), Skassy Kasambula amerejea nchini baada ya kutokuwepo takriban miaka 28.

Skassy ambaye alipigia OSS katikati ya miaka ya 1980 kwa vipindi vya mitindo ya Dukuduku, iliyokuwa ikiongozwa na Freddie Ndala Kasheba, na Ndekule iliyokuwa ikiongozwa na Muhidini Maalim Gurumo ambayo wote ni marehemu, yupo Dodoma akiendelea na kazi ya muziki.

"Nipo nchini Tanzania, nimerejea baada ya takriban miaka 28 hivi, kwa miaka yote hii nilikuwa nipo nchini Kenya nikiendelea na kazi hii ya muziki, lakini baada ya nchi kuzuia mikusanyiko kutokana na janga la COVID-19, niliondoka, nikaingia nchini hapa nikiwa Arusha ambako nimekaa sana na sasa nimesogea Dodoma," alisema mwanamuziki huyo ambaye ametunga na kuimba nyimbo nyingi ikiwemo 'Mama Belly' akiwa na Super Matimila na 'Christina Moshi', akiwa na OSS ya Ndekule.

Skassy, ameahidi kwenda Tanga na hatimaye kutua jijini Dar es Salaam kwa ajili ya muziki pamoja na kuisalimia familia yake iliyopo jijini, huku pia akiahidi kufanya ziara kwenye vyombo mbalimbali vya habari.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BELLINGHMAN ANUKIA MADRID

REAL Madrid iko tayari kutangaza hatua yao ya kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 kutoka Borussia Dortmund wiki ijayo. (***Marca***)

### RICE AICHAGUA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, angependelea kujiunga na Arsenal msimu huu, huku Manchester United, Chelsea na Bayern Munich pia zikiwania huduma ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. (***Mirror***)

### MOUNT KUIKAMUA UNITED

KLABU ya Manchester United bado haijakidhi kiwango cha Chelsea cha pauni milioni 55 ambayo ndio thamani waliyompa kiungo wa kati wa England, Mason Mount, licha ya kuongoza mbio za kinyang'anyiro cha kumchukua mchezaji huyo. (***Independent***)

### CHELSEA KUMUUZA MENDY

CHELSEA inaangalia jinsi ya kumuuza mmoja wa makipa wake, huku mchezaji wa kimataifa wa Senegal, Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 31 akitajwa kuwa na uwezekano mkubwa wa kuondoka katika klabu hiyo msimu huu . (***90min***)

### SZOBOSZLAI KUTUA EPL

KLABU ya Newcastle United imewatuma waangalizi wao kumfuatilia kwa karibu kiungo wa RB Leipzig na Hungary, Dominik Szoboszlai, mwenye umri wa miaka 22, mara mbili katika kipindi cha wiki mbili. (***Sky Sports***)

### CITY YAMTAKA CANCELO

MANCHESTER City ipo tayari kutoa kitita cha euro milioni 40 zinazohitajika kama gharama ya kumnunua beki wa Ureno, Joao Cancelo (28), ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo katika klabu ya Bayern Munich, huku Barcelona pia wakionyesha kumhitaji mchezaji huyo. (***Sport***)

### ASENSIO KUONDOKA MADRID

MARCO Asensio yuko tayari kuondoka Real Madrid wakati mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu baada ya mazungumzo baina ya klabu hiyo na kiungo huyo wa kati wa Hispania mwenye umri wa miaka 27 kugonga mwamba. (***Athletic***)

### RAYA ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inaongoza katika mbio za kununua mlinda mlango wa Brentford na Timu ya Taifa ya Hispania, David Raya, mwenye umri wa miaka 27. (***GiveMesport***)

### BRENTFORD, FLEKKEN SAFI

GOLIKIPA wa SC Freiburg na Uholanzi, Mark Flekken, anakaribia kutia saini mkataba kwa ajili ya kujiunga na Brentford, huku klabu hiyo ya Ligi Kuu England ikiwa tayari kurefusha mkataba na mchezaji huyo wenye kipengele cha kumwachia cha euro milioni 13. (***Sky Sports***)

### WEST YAMTAKA TAVARES

KLABU ya West Ham inamtaka beki wa Arsenal, Nuno Tavares, mwenye umri wa miaka 23, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo katika klabu ya Marseille. (***Record***)

### SPURS, DAVIES KUTETA

TOTTENHAM Hotspur iko tayari kusikiliza ofa ya mlinzi wa Timu ya Taifa ya Wales mwenye umri wa miaka 30, Ben Davies, kwa ajili ya msimu mpya. (***Football Insider***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP : SIHOFII SALAH KUONDOKA

### Kocha huyo pia afunguka Liverpool kushindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa ni...

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, haamini Mohamed Salah, atatafuta njia ya kuondoka ili kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Akiandika kwenye mitandao ya kijamii baada ya ushindi wa Manchester United dhidi ya Chelsea Alhamisi iliyopita na kuwafanya Liverpool kudondokea kwenye Ligi ya Europa msimu ujao, fowadi huyo wa Misri alisema "nimehuzunishwa" na "hakuna kisingizio" cha kutomaliza katika nafasi nne bora kwenye Ligi ya Kuu England.

Majira ya joto yaliyopita mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alisaini mkataba mpya na kumfanya kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi katika historia ya klabu hiyo.

Alipoulizwa kama ana wasiwasi kuhusu mustakabali wa Salah baada ya taarifa yake ya nadra kwa umma, Klopp alisema: "Hakuna wasiwasi, hapana. Nilisikia tu alichosema lakini sikuweza kusoma chochote.

**"Ni wazi Mo anapenda kuwa hapa na Mo alikuwa sehemu yetu. Alisema anaomba msamaha kwa kile 'sisi' tulifanya - sio kuomba msamaha kwa 'kile ambacho watu wengine walifanya.**

"Kama kuna mchezaji angenijia na kusema, 'Lo, hatukufuzu Ligi ya Mabingwa, lazima niondoke', ningempeleka kwenye klabu nyingine mwenyewe.

"Ningechukua ufunguo, (na kusema) 'njoo kwenye gari, unataka kwenda wapi, ninakuendesha'.

"Hilo lingekuwa jambo ambalo sikuweza kuelewa. Ningesema, 'oh, hatukufuzu kwa Ligi ya Mabingwa, nahitaji kufanya kazi kwenye Ligi ya Mabingwa ili niende'."

Klopp alisema kama huo ni mtazamo anaoukubali yeye pia atataka kuondoka.

"Ninawajibika kwa hii au chochote, kwa hiyo," aliongeza.

Kushindwa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa kunatazamiwa kuigharimu Liverpool angalau pauni milioni 50 msimu ujao

Klabu hiyo tayari imejiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua kiungo wa kati wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham, baada ya bei yake kuwa juu, na ripoti za wiki hii zilisema kiungo wa Chelsea, Mason Mount anapendelea kwenda Manchester United.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
FULHAM
1 | 1.56
X | 4.19
2 | 4.79

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LAMPARD: KOCHA MPYA ATAIBADILISHA CHELSEA



**LONDON,** England

FRANK Lampard amesema kubadilisha matokeo ya Chelsea litakuwa tatizo la kocha anayefuata anapojiandaa kuachia nafasi yake ya muda baada ya mchezo wa leo dhidi ya Newcastle United.

Msimu mbaya wa timu hiyo ulidorora kwa kipigo cha mabao 4-1 dhidi ya Manchester United kwenye Uwanja wa Old Trafford Alhamisi iliyopita kikiwa ni kipigo cha tisa kati ya michezo 11 ya Lampard.

Ikiwa matokeo yatawakabili siku ya mwisho wanaweza kumaliza wakiwa chini hadi nafasi ya 14 na kuwa katika nafasi mbaya zaidi katika zama za Ligi Kuu England.

Tayari wana uhakika wa kumaliza na pointi zao za chini zaidi kwenye kinyang'anyiro hicho, huku wakiwa na idadi ndogo ya mabao ambayo klabu hiyo imefunga kwenye msimu huu.

Mauricio Pochettino anatarajiwa kuteuliwa kuwa kocha ajaye wa kudumu wa klabu hiyo katika siku zijazo na ana kazi ya kutengeneza kikosi cha ushindi ambacho kilipotea njia tangu Graham Potter alipotimuliwa mwezi uliopita.

"Sijui," alisema Lampard. "Inabaki kuonekana, siwezi kuruka katika siku zijazo.

"Nadhani ni kazi nzuri kwa sababu ni kazi ya Chelsea na nilipoichukua mara ya kwanza (mwaka 2019) nilipokuja labda niliipata kwa sababu wasimamizi wengi wa juu hawakutaka hiyo.

# Asensio akaribia kutua PSG




**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Marco Asensio, yuko katika mazungumzo ya juu ya kujiunga na Paris Saint-Germain kama mchezaji huru, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mhispania huyo ambaye mkataba wake unamalizika majira ya joto, alipokea pendekezo la kuongezwa upya na Madrid ambalo lilimshawishi kifedha lakini ameamua kuhama baada ya msimu ambao ameanza chini ya nusu ya michezo ya klabu hiyo ya LaLiga.

Vyanzo viliiambia ESPN Aston Villa, Juventus na AC Milan pia zimeonyesha nia ya kumtaka katika miezi ya hivi karibuni, lakini pendekezo la PSG kwa sasa ndilo linalomvutia zaidi Asensio.

Uhusiano mzuri kati ya Jorge Mendes, wakala wa Asensio, na Luis Campos, Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, umekuwa muhimu katika mazungumzo hayo, vyanzo viliongeza.

PSG wanapanga kufanya marekebisho katika majira ya joto ambayo yatajumuisha kuondoka kwa Lionel Messi na kuajiri kocha kuchukua nafasi ya Christophe Galtier.

Timu hiyo pia inataka kuachana na Neymar na inatafuta mshambuliaji wa kuendamana na Kylian Mbappe katika safu ya mashambulizi, vyanzo hivyo vilisema.

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# CECAFA U-18 WASICHANA KUFANYIKA KENYA JUNI 24

**Na Saada Akida**

MASHINDANO ya soka ya wasichana wa umri chini ya miaka 18 ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-18) sasa yatafanyika kuanzia Juni 24 hadi Julai 8, mwaka huu jijini Nairobi, Kenya.

Awali mashindano hayo yalipangwa kuanzia kuanzia Juni 3 hadi Juni 17, mwaka huu huko huko Kenya.

Mashindano hayo yanayotarajiwa kushirikisha nchi wanachama wa CECAFA yanafanyika ili kupata mwakilishi wa ukanda huu atakayeshiriki kwenye fainali za Afrika zitakazochezwa baadaye mwaka huu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Auka Gacheo, alisema maandalizi ya mashindano hayo yanaendelea vyema na wanaamini timu zitaonyesha ushindani na hatimaye kupata mwakilishi imara.

Gacheo alisema wanaendelea kuilishukuru Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa kuendelea kuendesha mashindano ya wanawake na kupitia michuano hiyo, wasichana wanapata nafasi ya kuonyesha na kukuza vipaji vyao.

"Mashindano ya CECAFA U-18 sasa yatafanyika kuanzia Juni 24, yamesogea mbele kidogo ili kukamilisha maandalizi, tunahitaji kuwa na mashindano mazuri na yenye mafanikio," alisema Gacheo.

Timu ya wasichana ya Tanzania itakayoshiriki mashindano hayo iaendelea na mazoezi chini ya Kocha Mkuu, Bakari Shime.



Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mpira wa Miguu wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Mohammed Sidat (wa pili kushoto) akizungumza na Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Leodeger Tenga, Katibu Mkuu wa TFF, Kidao Wilfred (kulia) baada ya kufunga Warsha ya mafunzo ya Leseni za Klabu iliyojumuisha washiriki kutoka nchi 17 barani hapa. **PICHA: TFF**

# *Ni siku ya Yanga*

INATOKA UK. 24

mazuri, " alisema Kocha huyo.

Wakati huo huo, imeelezwa Yanga imefika fainali kutokana na hamasa kubwa iliyoongozwa na Rais Samia, alianza kununua kila goli lililofungwa kwa Sh. milioni tano kwenye hatua ya makundi ya kuwakafanya wanafainali hawa kuvuna Sh. milioni 95.

"Mimi kama Rais wa Tanzania nipo mstari wa mbele kwenye vita hii nikiwa na hamu ya kuona timu yetu inafanya vizuri kimataifa, hivyo pamoja na mambo mengine, naomba tuisapoti timu yetu kwa nguvu zote ili ifanye vizuri," alisema Rais Samia hivi karibuni.

Naye Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema ahadi ya kwanza ya Rais Samia ya Sh. milioni 20 kila bao watakalofunga katika mechi ya leo iko pale pale.

Msigwa alisema ahadi ya pili ni kutoa tiketi 5,000 ambazo thamani yake ni Sh. milioni 25 inalenga kuhamasisha mashabiki kuingia uwanjani kwa ajili ya kushuhudia fainali hiyo.

"Lakini pia mama aliahidi kutoa ndege ambayo iko tayari kwa safari ya kwenda Algeria katika mchezo wa marudiano, kikubwa Mh Rais (Samia), amewatakia kila la kheri wachezaji kwa ajili ya mchezo wa kesho (leo) kufanya vizuri," alisema Msigwa.

# USM Alger hatari kwa kona, beki...

INATOKA UK. 24

lakini ilikuwa kwanza ni kona iliyopigwa na Waarabu hao na Allan Katerega wa St. Eloi Lupopo alijifunga.

Yanga imefunga bao moja tu la mkwaju wa faulo kwenye mechi ya nyumbani iliyocheza dhidi ya TP Mazembe, kupitia Kennedy Musonda, aliyefunga kwa kichwa akiunganisha mpira wa faulo iliyopigwa na Djuma Shaaban, lakini wapinzani wao wamefunga mabao mawili kwa mikwaju hiyo ya kutenga.

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 28/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3989 | Verona vs Empoli | 1.67 | 3.66 | 4.62 |
| 15:00 | 2143 | Tusker vs Gor Mahia | 2.20 | 3.00 | 3.00 |
| 15:00 | 5266 | Shakhtar Donetsk vs SC Dnipro 1 | 1.85 | 3.48 | 3.53 |
| 15:15 | 3309 | FC Talanta vs KK Homeboyz | 2.80 | 2.90 | 2.40 |
| 15:30 | 1272 | Cambuur vs Waalwick | 3.30 | 3.75 | 1.92 |
| 15:30 | 1384 | Heerenveen vs GO Ahead Eagles | 2.03 | 3.71 | 3.06 |
| 15:30 | 1676 | Groningen vs Sparta Rotterdam | 3.05 | 3.40 | 2.13 |
| 15:30 | 2122 | Feyenoord vs Vitesse Arnhem | 1.26 | 5.81 | 8.01 |
| 15:30 | 2260 | FC Volendam vs SBV Excelsior | 1.70 | 4.20 | 3.80 |
| 15:30 | 2782 | Fortuna Sittard vs NEC Nijmegen | 2.47 | 3.50 | 2.50 |
| 15:30 | 3984 | Carlisle vs Stockport | 2.88 | 3.13 | 2.31 |
| 15:30 | 4406 | Twente vs Ajax | 3.75 | 4.01 | 1.74 |
| 15:30 | 5727 | AZ Alkmaar vs PSV Eindhoven | 2.55 | 3.61 | 2.37 |
| 15:30 | 5986 | Utrecht vs Emmen | 1.49 | 4.40 | 5.20 |
| 16:00 | 1448 | Bologna vs Napoli | 3.15 | 3.15 | 2.20 |
| 16:00 | 1550 | Monza vs Lecce | 2.39 | 3.11 | 2.85 |
| 16:30 | 1232 | Magdeburg vs Arminia Bielefeld | 3.03 | 3.83 | 2.05 |
| 16:30 | 1948 | Sandhausen vs Hamburger SV | 6.66 | 5.25 | 1.35 |
| 16:30 | 2117 | St. Pauli vs Karlsruher SC | 1.83 | 3.87 | 3.62 |
| 16:30 | 2649 | Kaiserslautern vs Fortuna Dusseldorf | 2.52 | 3.49 | 2.53 |
| 16:30 | 3931 | Jahn Regensburg vs Heidenheim | 5.64 | 4.33 | 1.49 |
| 16:30 | 4278 | Hannover vs Holstein Kiel | 2.16 | 3.73 | 2.87 |
| 16:30 | 5608 | Hansa vs Eintracht Braunschweig | 2.51 | 3.39 | 2.58 |
| 16:30 | 5680 | Greuther Furth vs SV Darmstadt | 2.63 | 3.34 | 2.50 |
| 16:30 | 5831 | Paderborn vs Nurnberg | 1.94 | 3.73 | 3.38 |
| 17:00 | 1694 | St Johnstone vs Livingston | 2.22 | 3.10 | 3.20 |
| 17:15 | 1210 | Racing Santander vs FC Cartagena | 2.64 | 3.14 | 2.54 |
| 17:30 | 1996 | Nacional Madeira vs Viseu | 2.13 | 3.33 | 3.07 |
| 17:30 | 3745 | CD Trofense vs Mafra | 1.91 | 3.38 | 3.64 |
| 18:30 | 1859 | Arsenal vs Wolverhampton | 1.39 | 4.67 | 6.36 |
| 18:30 | 2512 | Leeds vs Tottenham | 2.65 | 3.59 | 2.31 |
| 18:30 | 2874 | Everton vs Bournemouth | 1.43 | 4.41 | 6.02 |
| 18:30 | 3528 | Leicester vs West Ham | 1.89 | 3.70 | 3.45 |
| 18:30 | 4022 | Aston Villa vs Brighton | 2.00 | 3.66 | 3.16 |
| 18:30 | 4067 | Brentford vs Manchester City | 3.52 | 3.62 | 1.89 |
| 18:30 | 4103 | Southampton vs Liverpool | 5.81 | 4.68 | 1.42 |
| 18:30 | 5258 | Manchester Utd vs Fulham | 1.56 | 4.19 | 4.76 |
| 18:30 | 5323 | Chelsea vs Newcastle | 2.70 | 3.35 | 2.37 |
| 18:30 | 5575 | Crystal Palace vs Nottingham | 1.65 | 3.86 | 4.41 |
| 19:00 | 5187 | Lazio vs Cremonese | 1.21 | 5.80 | 11.00 |
| 20:00 | 1017 | Athletic Bilbao vs Elche | 1.31 | 4.91 | 8.02 |
| 20:00 | 1633 | Atletico Madrid vs Real Sociedad | 2.01 | 3.35 | 3.40 |
| 20:00 | 1737 | Valencia vs Espanyol | 2.10 | 3.36 | 3.16 |
| 20:00 | 2756 | Almeria vs Valladolid | 2.24 | 3.35 | 2.90 |
| 20:00 | 2788 | Barcelona vs Mallorca | 1.34 | 4.78 | 7.37 |
| 20:00 | 2949 | Rayo Vallecano vs Villarreal | 2.85 | 3.40 | 2.24 |
| 20:00 | 2984 | Girona vs Betis | 2.00 | 3.44 | 3.35 |
| 20:00 | 3804 | Cadiz CF vs Celta Vigo | 2.54 | 3.14 | 2.64 |
| 20:00 | 4835 | Getafe vs Osasuna | 2.07 | 3.15 | 3.45 |
| 21:45 | 4494 | Juventus vs AC Milan | 2.35 | 3.17 | 2.87 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Mei 28, 2023
Nipashe



UK. 21

## Klopp : Sihofii Salah kuondoka



Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa (kulia), akikabidhi Sh. milioni 25 kwa ajili ya kulipia tiketi 5,000 zilizonunuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ili kuwapa mashabiki kushuhudia fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika kati ya Yanga dhidi ya USM Alger itakayochezwa leo. Kushoto ni beki wa timu hiyo, Dickson Job na Ofisa Habari, Ali Kamwe. **PICHA: MTANDAO**

# Ni siku ya Yanga

**Na Saada Akida**

## ●●● Hamasa za Rais Samia zawabeba, awatakia heri huku Bangala...

BAADA ya miaka 30 kupita, timu ya Tanzania, wawakilishi hao pekee wa nchi waliobakia katika mashindano ya kimataifa wanawakaribisha USM Alger kutoka Algeria katika mechi ya kwanza ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga ambayo inahitaji kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo ya mkondo wa kwanza itamkosa kiungo wake tegemeo, Khalid Aucho, raia wa Uganda kutokana na kutumikia adhabu ya kadi za njano alizozipata katika michuano hiyo.

Kuelekea mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema atafanya mabadiliko madogo katika safu ya kiungo baada ya kumkosa Aucho na kuweka wazi nafasi yake itachukuliwa na Yannick Bangala ambaye aliwahi kucheza fainali ya CAF mwaka 2018, kabla ya kusajiliwa na Yanga.

Nabi alisema wamefanya maandalizi katika sehemu kuu tatu kwa ajili ya kupata matokeo mazuri ikiwamo kufahamu wapinzani wao wanavyocheza wanapokuwa ugenini.

"Kutokuwepo Aucho (Khalid) imetusikitisha kwa sababu alikuwa sehemu ya mchezo, ni pengo kubwa kiufundi, lakini hatuwezi kushindana na sheria, kuna wachezaji wazuri ikiwamo Yannick Bangala ambaye aliwahi kucheza fainali mwaka 2018, ninaimani atafanya vizuri," alisema Nabi.

Aliongeza anashukuru na kujivunia kuwa na namba tisa bora Afrika ndani ya kikosi chake ambaye ni Mayele (Fiston) lakini pia kuwa na kipa mzuri, beki na viungo wazuri ila mchezaji mmoja hawezi kuleta matokeo lazima kuwepo kwa ushirikiano.

"Wachezaji wetu wana molari na wana uwezo wa kuchukua ubingwa kwa sababu ni wazuri, naomba mashabiki kusimama na sisi katika dakika zote 180, dakika 90 za kesho (leo) nyumbani na dakika 90 za ugenini Algeria," aliongeza kocha huyo.

Aliongeza timu yake haitaingia katika mtengo wa kufunguka kama walivyocheza dhidi ya Al Hilal na hatimaye waliondolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na sasa wanashindana kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho.

Naye mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Dickson Job, alisema wamejipanga vizuri na wanaenda kupambana kuhakikisha wanafanya vyema katika mchezo huo kwa ajili ya heshima ya Tanzania.

"Tumejiandaa vizuri, tuko tayari kujitolea kupata matokeo mazuri, safu yetu ya ulinzi tumepata maelekezo mazuri na kila mchezaji anatambua umuhimu wa mchezo huu, kila mmoja wetu tunahitaji kuona tumefanya vizuri mechi ya nyumbani na tunapokwenda ugenini kumalizia ili kutwaa ubingwa wa Afrika," alisema Job.

Kocha wa USM Alger, Benchikha Abdelhak, alisema wanashukuru kufika hatua ya kucheza fainali hii na wachezaji wako tayari kwa mchezo huo.

"Tunatambua nchi nzima iko nyuma yetu kututizama, lakini kwa maandalizi tuliyofanya nina imani itakuwa fainali nzuri na kuhakikisha kupata matokeo mazuri ugenini. Unaweza kukosa hapa lakini ukafika nyumbani ukapata matokeo

INAENDELEA UK. 23

## USM Alger hatari kwa kona, beki...

**Na Adam Fungamwango**

SIKU imefika, Yanga inashuka dimbani leo kuwakaribisha USM Alger kutoka Algeria, pembeni mwa uwanja, kwani mabao yao wawakilishi hao pekee wa Afrika Mashariki na Kati, wanatakiwa kufahamu mabao tisa kati ya 17 ya wapinzani wao yamepatikana kutokea kwenye winga zao zote mbili.

Kati ya mabao hayo, matano yamefungwa kwa krosi na manne ni ya kona, hivyo benchi la ufundi la Yanga lina kazi ya kufanya kuzidhibiti maeneo hayo.

Yanga pia wanapaswa kujua wanakwenda kucheza na timu yenye kipa bora, Oussama Benbot, raia wa Algeria ambaye ndiye mhilimi kubwa na kikosi hicho akiokoa michomo mingi, akiisadia kwa kiasi kikubwa timu hiyo kufika hapo, huku ikiwa na udhaifu kidogo upande wao mabeki.

Kwa mujinu wa takwimu zetu ni, wakati Yanga ikiwa imefunga mabao 13 ndani ya eneo la hatari kati ya michezo 15 iliyocheza, USM Alger imefunga magoli mawili tu ndani ya eneo hilo kati ya magoli 17 waliofunga, hivyo kuonekana hawana hatari sana ndani ya eneo hasa mashambulizi yanapopitia katikati.

Mawinga wao Khaled Bousseliou akicheza kulia, na Abderrahmane Meziane akicheza kushoto huwa ni hatari, wakisaidiwa na mabeki wao wa kupanda na kushuka, Saadi Radouani upande wa kulia na Brahim Benzaza upande wa kushoto.

USM Alger ina bao moja tu ambalo imelipata kwa shuti la nje ya boksi ambalo lilipatikana Februari 26 kwenye mechi ya hatua ya makundi dhidi ya Marumo Gallants nchini Algeria ikishinda mabao 2-0.

Moja kati ya mabao ya USM Alger ni ya mchezaji wa timu pinzani kujifunga mwenyewe,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002